# MZOZO KANISANI KWA VARWA:

# 1990 - 1993

## Mtengano ndani ya Dayosisi ya Kilutheri ya Kaskazini mwa Tanzania

**Dr. Catherine Baroin**

(Kimetafsiriwa na Baltazari Z. Kaaya
na kuhaririwa na Justin E. Mungure)

**DIBAJI (Kwa toleo la Kiswahili)**

Andiko hili katika lugha ya Kiswahili limetafsiriwa kutoka andiko la awali katika lugha ya Kiingereza lililochapwa na Dr. Catherine Baroin mwaka 1996 kwa kichwa: "Religious Conflict in 1990-1993 Among the Rwa: Secession in a Lutheran Diocese in Northern Tanzania," na kutolewa katika gazeti la *African Affairs: The Journal of the Royal African Society*, vol. 95, no. 381, eds Peter Woodward & David Killingray. 529-554. Oxford: Oxford University College for The Royal African Society.

Nia ya kutoa tafsiri hii ya Kiswahili ni ili kuwawezesha wahusika wa matukio yaliyomo, ambao ni wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili, kuelewa yale yaliyoandikwa ndani yake.

Mwandishi Catherine Baroin (Nkamirisho) ni Mfaransa aliye mtafiti katika fani ya sayansi ya jamii. Yeye si Mtanzania na wala siyo Mlutheri wala si Mtheologia bali ni mtaftiti tu. Kwa sasa anaendelea na utafiti juu ya mabadiliko ya kijamii yanayotokea ndani ya kabila la Wameru (Varwa), kama yalivyo pia katika taifa zima.

Shukrani nyingi zimwendee mwandishi, Dr. Catherine Baroin, kwa andiko lake linalohifadhi habari inayohusu kanisa na jamii ya Tanzania. Pia shukrani zikiendee chama cha utafiti wa sayansi ya jamii cha Ufaransa (CNRS) na wachapishaji wa gazeti la *African Affairs: The Journal of the Royal African Society* wa London Kent, Uingereza kwa kuruhusu tafsiri hii ifanyike. Mwisho nawashukuru wote ambao kwa njia moja au nyingine wamewezesha tafsiri hii ikafanyika na kuchapishwa.

**Mfasiri - Mch. Baltazar Z. Kaaya, 2007**

## UTANGULIZI

Kutokana na makubaliano kati ya Wajerumani na Waingereza hapo mwaka wa 1886, Tanzania Bara (zamani Tanganyika) iliwekwa chini ya utawala wa Wajerumani wakati huo wa zama za awali za ukoloni.[1] Tokea wakati huo desturi na ushawishi mwingi kwa jamii zinazoishi katika Mlima Kilimanjaro, na pia Mlima Meru uliopo magharibi yake, vilitawaliwa sana na Kanisa la Kilutheri. Tokea mwishoni mwa karne ya 19 kanisa hili limekuwa likituma wamisionari, kwanza kule Kilimanjaro, na baadaye Mlima Meru. Licha ya ugumu kidogo hapo mwanzoni, Ulutheri ulienea kwa kasi na kwa mafanikio makubwa katika maeneo hayo. Kwa sasa hivi kanisa hili ndilo maarufu kwenye ukanda huu wa milima, kaskazini mwa Tanzania.

Tofauti kabisa na sehemu zingine za Afrika huru, Tanzania imekuwa ya pekee kwa amani na kutokuwa na mizozo ya ndani hadi pale Varwa, ambao huishi kwenye miteremko ya Mlima Meru, walipobatilisha hali hiyo hapo mwaka 1990 - 1993 kwenye mzozo ulioibuka ndani ya Kanisa la Kilutheri kati ya baadhi ya waumini waliotaka kujitenga na wale wa mrengo wa wachungaji ambao hawakupendelea kutengana. Kwa kitambo, mzozo huu ulivutia sana vyombo vya habari (huku vikilaumu) na kuandika juu ya kabila hili dogo lenye watu wapatao 150,000 wajulikanao kama Wameru wa Tanzania.[2] Katika lugha yao ya Ki-rwa, Wameru hawa hujiita Varwa, (N-rwa- umoja, na Va-rwa -

---

[1] John Iliffe, A *Modern Hhistory of Tanganyika* (Cambrige University Press, Cambridge, 1979).

[2] Paul Puritt, "The Meru of Tanzania: A Study of Their Social and Political Organization" (Unpublished Ph.D. University of Illinois, 1970). Paul Puritt, "The Meru of Northeastern Tanzania", katika Sally Falk Moore and Paul Puritt, *The Chagga and the Meru of Tanzania,* (International African Institute, Ethnographic Survey of Africa, 18, London, 1977) uk. 90 - 140.

wingi); na yafaa hapa kutowalinganisha kabisa na Wameru wa Kenya ambao hawana uhusiano wo wote.

Lengo la andiko hili ni kuelezea matukio muhimu, hatua kwa hatua, kwenye mzozo huu uliotokea ndani ya Kanisa la Kilutheri, kuelezea kwa undani chanzo na sababu zake, mamlaka za kijamii zilizohusika kwenye mzozo huu, na mwisho kuangalia matokeo ya mzozo huu hasa kwa jinsi gani ulivyogusa maisha na taasisi za kijamii ndani ya kabila la Varwa.

Hata hivyo ni muhimu kuelezea kwanza kiini cha mzozo huu kwa kuangalia vishawishi vikuu ndani yake: Serikali ya Tanzania na mfumo wake wa Siasa ya Ujamaa; Kanisa la Kilutheri la Tanzania; na mwisho kuangalia mhusika wake mkuu, kabila la Varwa.

## HALI ILIVYOKUWA KABLA YA MATUKIO YA MZOZO

### (i) Tanzania na Serikali yake

Serikali ya Tanzania, bila kujijua, ilichangia sana kwenye mzozo huu. Serikali hii ilichukulia mambo kwa kufuata mawazo ya siasa ya Ujamaa ya Julius Nyerere ambaye hadi leo bado anaheshimika sana nchini Tanzania. Siasa hii inadhihirika wazi kwa mkazo wake wa kuhimiza kujitegemea, elimu kwa wote, huduma bure za afya na usawa wa binadamu. Elimu, ambayo hutolewa kwa lugha ya Kiswahili kwenye shule zote za msingi, imewawezesha karibu watu wote kufahamu Kiswahili ambacho huzungumzwa karibu na kila mtu Tanzania. Kiswahili kimekuwa kiungo muhimu kwa Watanzania wote ambao ni muunganiko wa makabila zaidi ya mia moja na ishirini.[3] Elimu ya Demokrasia iliwekewa mkazo sana mashuleni; na sasa maamuzi mengi hufanywa na kutekelezwa kwa kufuata mtindo wa kidemokrasia wa kura ya wengi. Katika mikutano, idadi itakiwayo ya wajumbe (koramu) ni kitu muhimu cha kuzingatiwa, baada ya kumpata mwenyekiti na katibu wa mkutano. Mtindo huu ulionekana kufuatwa katika kufikia baadhi ya maamuzi muhimu yaliyoasilishwa na mzozo huu.

Ujamaa wa Tanzania hujidhihirisha pia kwa njia ya silika yake ya uvumivu kama inayoonekana kwenye uhuru wa kuabudu unaoelezwa pia kwenye katiba. Roho ya kuvumiliana ilionekana pia katika itikadi ya kupambana dhidi ya “ukabila” ambao wengi huamini kuwa ni hatari kwa utulivu wa kitaifa.

---

[3] Denis-Constant Martin,' Le pouvoir en discussion. Etat, structures sociales et culture politique en Tanzania'
(University of Paris V, these pour le doctoral d'Etat es-lettres, 1987). Herman Batibo and Denis-Constant Martin (ed), *Tanzanie - L'ujamaa face aux r£a\Ms* (Editions Recherche sur les Civilisations, Memoire No. 80, Paris, 1989).

"Ukabila" una tafsiri finyu, ya kinyume, hapa Tanzania, na tuhuma dhidi ya ukabila, kama mifano inavyoonyesha hapa chini, ni jambo lililo baya sana. Hata hivyo makabila bado yapo Tanzania na hata mgawanyiko wa sharika na majimbo kikanisa hufuata kabila fulani hasa kwa Walutheri.[4] Japo mahubiri kanisani mara nyingi hutolewa kwa Kiswahili, nyimbo nyingi huimbwa kwa kilugha (hapa Kirwa) na ambapo Wamisionari wa Kilutheri walitafsiri maandiko na vitabu vingi vya kidini kwa lugha za wenyeji husika.

Roho ya kuvumiliana ambayo inatawala Tanzania ilionekana, japo wakati mwingine kwa muda mfupi tu, kwenye uhuru wa vyombo vya habari. Hata hivyo uthibiti na matumizi ya vyombo vya habari ambavyo huhitaji fedha nyingi ambazo Watanzania wengi hawana, ulibaki kwenye ukiritimba wa Serikali, Chama tawala na Kanisa. Hali hii ilijidhihirisha wazi kwenye mzozo huu kama tutakavyoelezea, ambapo iliwaathiri sana wale Walutheri waliotaka kujitenga kutokana na uwezo na sauti yao kuwa ndogo kwenye vyombo hivyo vya habari.

Ni vyema kuelewa kuwa licha ya kuwepo elimu ya demokrasia na roho ya kuvumiliana bado Chama Cha Mapinduzi (C.C.M.) kina nguvu kubwa na nafasi ya kipekee katika nchi hii, licha ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa hivi karibuni. Upekee huo wa Chama hiki si jambo la kushangaza kutoka na ukweli juu ya umaaraufu na utendaji wake. Katika utawala wa nchi, maeneo yake yamegawanywa kwenye mikoa, wilaya, tarafa, kata na vijiji. Mfumo huu ulirithiwa toka utawala wa Kikoloni. Kijiji nacho hugawanywa zaidi kwenye mashina ya nyumba (kaya) kumi

---

[4] M. Vahakangas, 'Etnincn Identiteetti kuohuttaa kirkkoa Tansaniassa', *Suomen Lahetyssanomat (*Finland) 3 (1993), uk. 26-29.

chini ya kiongozi wa shina ambaye hujulikana kama ‘balozi’ wa nyumba kumi. Kwa sasa kila Kijiji kimegawanywa tena katika vitongoji ambapo kila kitongoji huwa na wastani wa kaya hamsini. Katika kila ngazi ya utawala kuna ushirikiano wa karibu sana kwa viongozi wa Serikali na Chama.

Mwisho, ni muhimu kusisitiza kuwa itikadi ya Kijamaa, ambayo bado ipo nchini, huenda sambamba na hali duni ya maendeleo iliyopo, pia nchi kwa jumla ni maskini (ingawa kaskazini mwa nchi penye mzozo huu kuna utajiri mwingi). Hali hii duni ya maendeleo isiyoridhisha, ambayo husababisha pia tamaa za hongo, huleta mgawanyo hafifu wa miundo mbinu ya nchi jambo ambalo linaonekana hata kwenye mzozo huu wa kidini. Hali hii duni ya uchumi, ukosefu wa ajira, pamoja na mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana ni mambo ambayo yanaonekana kuchochea mzozo huu.

### (ii) Kanisa la Kilutheri Tanzania

Kama ilivyoelezwa awali, Kanisa la Kilutheri ndilo la muda mrefu zaidi kuanzishwa katika maeneo ya Kilimanjaro na Mlima Meru kaskazini mwa Tanzania. Pia ndilo kanisa lenye nguvu kuliko mengine yote. Ilikuwa mwaka wa 1892 ndipo chama cha Misioni cha Kilutheri cha Leipzig kilipoanza kazi huko Kilimanjaro. Mnamo mwaka wa 1896 chama hiki kilituma wamisionari wawili kwa Varwa, kule Akeri; lakini Varwa, kwa kuhofia ukoloni wa Wajerumani, waliwaua wamisionari hawa hapo tarehe 18 Oktoba 1896. Mwanzo huu mgumu ulicheleweshа kuanzishwa Ulutheri katika eneo la Varwa kwa miaka kadhaa japo tukio hili bila shaka liliongeza shauku ya

kueneza Injili katika eneo hili kwa kuwaenzi kama mashujaa wafia dini hao wawili.

Misioni ya Kilutheri ilianzishwa pale Nkoaranga mwaka 1902, katikati ya nchi ya Varwa. Hapo mwaka 1903, misioni mbili zilifunguliwa kule Akeri na Ngyani. Mwaka 1904 waumini wa kwanza walibatizwa kule Nkoaranga. Kazi ya kuhubiri injili kwa watu wengi zadi ilipata nguvu hasa kutokana na kwamba Wamisionari wa Kilutheri hawakubakia kwenye kuhubiri ya injili pekee, bali walifungua shule ya watoto na kuanzisha huduma za afya na matibabu kule Nkoaranga. Wanafunzi wa shule hii ya misioni walilima kwenye shamba la misioni la kahawa wakati wa mchana (na hapo ukawa mwanzo wa upandaji wa zao la kahawa kwa Varwa), na walikuwa wakipewa malipo ya shilingi moja kwa mwezi ambazo zilikuwa nyingi sana kwa wakati huo (ukichukulia kuwa dume moja la ng'ombe liligharimu shillingi tano tu).[5] Hatua hii ya malipo ya fedha iliwavutia wenyeji wengi kujiunga na kanisa ingawa kitendo cha kanisa kupinga baadhi ya mila za Varwa, kama vile kuwa na wake wengi (mitara) na unywaji wa pombe, kilileta upinzani na mgongano kwa muda mrefu.

Kutafsiriwa kwa vitabu vya Biblia na nyimbo za Kikristo katika lugha ya Kirwa kulitoa mchango mkubwa sana katika kuimarisha kanisa. Kwa mfano, mnamo mwaka 1964, Agano Jipya (Mma Shiyya) lilitafsiriwa na kuchapishwa kwa Kirwa na chama cha Misioni ya Kiinjili ya Kilutheri cha Leipzig. Kwa njia hii, kanisa la Kilutheri lilikua na kuimarika sana miongoni mwa Varwa kama ilivyokuwa sehemu nyingine nyingi nchini Tanzania.[6]

---

[5] A.S.Mbise, 'The Evangelist Matayo Leveriya Kaaya', katika John Diffe (ed), *Modern Tanzanians-a volume of biographies* (East African Publishing House, Nairobi, 1973), uk. 27-42.

[6] C.K Omari, 'Episcopacy: A Sociological Trend in the Lutheran Church in Tanzania', *Africa Theological Journal,* Makumira (Tanzania), 16 (1987), uk. 4 -12.

Mwaka 1963 Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (K.K.K.T) lilizaliwa kwa kuunganishwa kwa makanisa madogo madogo saba. Idadi ya Dayosisi za kanisa hili ilizidi kuongezeka kwa jinsi Wakristo walivyoongezeka. Kwa mfano, awali kulikuwa na Dayosisi moja kubwa ya Kaskazini ambayo mwaka 1972 iligawanyika na kuzaliwa dayosisi tatu zikiwa ni Pare, Arusha Mkoani na Kaskazini. Dayosisi hii mpya ya Kaskazini, na iliyo ndogo zaidi, ndiyo inayotuhusu hapa. Kujitenga kwa Sinodi ya Arusha Mkoani, ambayo sasa ni Dayosisi, kutoka Dayosisi ile kubwa ya Kaskazini, kulitokea kwa shari; kulitokea kwa njia ya mtengano japo baadaye kulipata ridhaa ya Kanisa (KKKT). Kwa njia moja au nyingine, kujitenga kwa Varwa kulikuwa marejeo ya historia ya nyuma kama ambayo tunataka kuelezea hapa. Hata hivyo, yafaa ikumbukwe kwamba hapo mwaka 1972, Varwa waliamua kubaki katika Dayosisi ya Kaskazini ambayo ina wingi wa Wachagga.[7] Uamuzi huu wa kubaki katika Dayosisi ya Kaskazini ulifikiwa katika kikao cha Halmashauri Kuu ya Jimbo la Meru mnamo tarehe 13 Julai 1972 kule Akeri. Tokea hapo, Dayosisi ya Kaskazini ilijigawa katika Majimbo sita: Meru, Karatu, Hai Magharibi, Hai Mashariki, Kilimanjaro Kati na Kilimanjaro Mashariki. Hadi kufikia mwaka 1990, Dayosisi hii ya Kaskazini ilikuwa na waumini wapatao 360, 000, ambapo asilimia ishirini kati yao, yaani waumini 83,000, walikuwa Varwa watokao katika Jimbo la Meru. Idadi kubwa ya waumini kwenye majimbo hayo mengine ni Wachagga.

Wakaaji wa Jimbo la Meru kwa ujumla ni Varwa, na Jimbo lina sharika zipatazo thelathini na tano ambapo mipaka ya sharika hizi haifuati moja kwa moja mipaka ya utawala wa

[7] Moore and Puritt, The Chagga and the Meru of Tanzania.

Serikali. Hivyo ni vigumu kulinganisha idadi ya watu katika sensa ya Serikali ya mwaka 1988 na idadi iliyotolewa na kanisa hili la Kilutheri ya waumini wake. Hata hivyo ni wazi kuwa katika eneo hili lenye makabila na sehemu mchanganyiko, yaani mijini na ukanda wa chini, Walutheri ndio wengi, wakiwa ni zaidi ya nusu ya wakaaji wote. Katika eneo la asili la Varwa, ambalo ni kusini Mashariki mwa Mlima Meru, Kanisa hili la Kilutheri ndilo lililotawala. Kuna baadhi ya madhehebu mengine ya Kiprotestanti ambayo katika siku za hivi karibuni yameanza kujiimarisha huko; Wabaptisti tangu mwaka 1966, na Wapentekoste tangu mwaka 1968 wakiwa na idadi ndogo tu ya waumini wao.[8] Hata hivyo idadi na ushawishi wa madhehebu haya mengine vimeongezeka kufuatia mzozo huu ambapo baadhi ya waumini wa Kilutheri wamehamia kwenye madhehebu haya.

Kanisa la Kilutheri kwa Varwa si maarufu tu kwa ukubwa na idadi ya waumini wake, bali pia linasimamia na kutawala karibu miundombinu yote muhimu. Licha ya kuwa na majengo ya makanisa, ardhi, na mashamba ya kahawa ambayo hulipatia fedha nyingi, kanisa hili linamiliki shule nne za Sekondari, vyuo vya mafunzo viwili yaani Chuo cha Ufundi cha Leguriki, kilichozinduliwa mwaka 1984, na chuo cha Mafunzo kwa wenye Ulemavu Usa-River tangu 1991, pamoja na hospitali pekee Jimboni ya Nkoaranga. Waumini ndio wanaobeba gharama za ujenzi wa majengo hayo yote, na kanisa hujishughulisha na utawala wa taasisi hizo na pia kutafuta au kuelimisha waalimu, pamoja na kutafuta fedha za uendeshaji na

[8] S.E Nnko, 'The Interdenominational Conflicts Within the Meru District of the ELCT - Northern Diocese' (Makerere University, unpublished Diploma of theology, Archives of the Makumira Lutheran Theological College in Tanzania, 1980).

kununulia vifaa vya elimu au vya hospitali na vyombo vingine vinavyohitajika.

Ni jambo la kushukuru kwamba Kanisa la Kilutheri hupata misaada mingi toka kwa wafadhili wa ng'ambo ambayo ni muhimu sana si kwa kanisa tu bali hata kwa nchi. Misaada ya fedha hizo huwezesha Kanisa hili kuchangia si kwenye elimu au afya tu bali pia kuchangia kwenye miradi mingine ya maendeleo kama miradi ya maji, kwa mfano kule Akeri na Urisho. Ni ukweli usiopingika kuwa Kanisa la Kilutheri katika ukanda huu wa Varwa limejijengea uimara na umaarufu mkubwa siyo kidini tu bali hata kiutawala, mithili ya dola ndani ya dola.

Umaarufu wa Kanisa hili unajidhihirisha pia kwa kuwatazama watumishi wake. Heshima ya mchungaji katika jamii yaweza kuwa ni zaidi hata kuliko ile anayopewa mshili wa ukoo, au hata mshili wa rika, na kwamba Kanisa laweza kumteuwa yeyote limpendalo kwenda kusomea uchungaji bila upinzani wowote. Wale waliochaguliwa hulipiwa na Kanisa gharama zote za masomo yao kwa muda wa miaka mitano. Kuhusu Askofu wa Dayosisi, yeye ni mtu mashuhuri na mheshimiwa kweli kweli. Katika nchi kama hii ambapo usafiri ni tatizo kubwa, yeye huwa na hadhi inayofanana na ile ya mbunge au waziri, hupewa gari zuri la kifahari lenye mitambo yenye kiyoyozi na kitia joto, tena lenye uendeshaji maalum kwa barabara zote. Umaarufu na ushawishi huu wa Kanisa la Kilutheri kwenye masuala ya kiroho na kijamii katika jamii ya Varwa ni changamoto tosha inayoelezea sababu zilizochocheo kuibuka kwa mzozo huu katika ngazi ya chini.

**(iii) Kabila la Varwa**

Varwa, ambao ni Wabantu wapatao 150,000, ni wakulima waishio mashariki na kusini mwa Mlima Meru (mita 4585) ulio magharibi mwa Mlima Kilimanjaro. Ardhi kwenye milima hii ni yenye rutuba na mvua nyingi ambapo hufaa sana kwa kilimo. Ndizi na kahawa (zao la biashara) ndiyo mazao yanayostawishwa kwa wingi. Wengi wa Wachagga waishio Kilimanjaro hutumia zaidi ndizi kama chakula chao kikuu, wakati ambapo Varwa hutumia zaidi mahindi kuliko ndizi. Pia Varwa hulima maharage kama zao lao la pili la biashara na hutumika kwa kuchanganywa kwenye vyakula mbalimbali pamoja na mazao mengine ambayo hulimwa kwa uchache zaidi. Tena karibu kila familia inayoishi kwenye eneo hili lenye watu wengi sana, hufuga angalau ng'ombe mmoja au wawili, pia kondoo na mbuzi kwenye mabanda na kuku wachache. Kila kaya huishi kwenye shamba lake yenyewe mbali na nyingine.

Kutokana na ongezeko la watu na kuzidi kubanana kwao, baadhi ya Varwa walianza kuhama tangu mwaka wa 1950 na kwenda kuishi kwenye ukanda wa tambarare mwa mlima Meru kusini na mashariki yake kwenye maeneo ya ufugaji ambayo ni makavu na hayana rutuba sana na hivyo kubadilisha kabisa aina ya kilimo huko na maisha kwa ujumla. Pamoja na kazi hizi za kilimo kumetokea ongezeko la kazi nyingine, kwa mfano, ufundi sadifu na mchundo, ualimu, biashara mbalimbali na hata pia kazi za muda zinazotokana na utalii kama vile udereva, makuli na waongozaji wa watalii kutokana na eneo hili kuwa karibu na mji wa Arusha ambao ni maarufu na makao makuu ya utalii Tanzania. Ingawa shughuli hizi humfanya mtu awe mbali na nyumbani kwao, hazimuondolei mtu utambulisho wake, Varwa wameunganishwa na lugha moja na pia wana utamaduni mmoja.

Kihistoria Varwa wana uhusiano na Wachagga wa Machame kule Kilimanjaro, na yasemekana kuwa wote ni wa uzao mmoja wa kundi la wahamiaji kwenye karne ya 17 waliotoka kwenye Milima ya Usambara iliyopo kilometa 250 kusini mashariki. Baadhi ya wahamiaji hao walilowea kwenye miteremko ya Mlima Meru na hapo ukawa ndio mwanzo wa Varwa (Varwa maana yake ni 'waliopanda'), na wengine walibaki na kulowea kule Kilimanjaro na huu ukawa ndio mwanzo wa Wamachame ambao desturi na lugha yao hufanana kwa karibu sana na zile za Varwa. Makabila haya mawili, Varwa na Wachagga, wana vitu vingi vinavyofanana: Wana mazingira yanayofanana, na kwa ujumla wana mtindo sawa wa maisha. Hata hivyo, Wachagga ni muunganiko wa makabila mengi madogo madogo, na ni wengi kama mara tisa zaidi kuliko Varwa; kwa mujibu wa takwimu za idadi ya watu katika sensa ya mwaka 1989 Wachagga walikuwa 700,000 ambapo Varwa walikuwa 80,000 tu.[9] Uhaba wa ardhi huwalazimisha baadhi ya Wachagga kuhama Kilimanjaro na kukimbilia maeneo mengine ya Tanzania. Tofauti na Varwa, Wachagga wanasifika sana kwa biashara; kwa ujumla wao ni wanamiji, wameelimika na ni matajiri zaidi kuliko Varwa. Haya yote hufanya Varwa kujihisi kuwa wako nyuma kimaendeleo kuliko Wachagga, jambo ambalo lilitosha kabisa kuwa sababu mojawapo ya kuibuka kwa mzozo huu kati yao.

Idadi kubwa ya Varwa ni waumini wa Kilutheri. Karibu wote wanajua kusoma, kuandika na kuongea Kiswahili ambacho ni lugha rasmi itumikayo kufundishia katika shule za msingi. Ni Varwa wachache tu wanaoelewa Kiingereza ambacho ni lugha itumikayo kufundishia katika shule za sekondari. Kirwa, ambacho ni lugha ya Varwa, nacho hutumika hata sasa ingawa kinamezwa

---

[9] Gerard Philippson, 'Les populations', in Batibo and Martin *Tanzanie - L'ujamaaface aux r£alit£s,* uk. 43.

na Kiswahili na hata vijana wengi wa Kirwa hawajui kabisa baadhi ya maneno ya kawaida kabisa ya lugha hii ya mama zao. Kutokana na mafundisho kuwa yuko Mungu mmoja, pamoja na elimu itolewayo kwa Kiswahili mashuleni na kuenea kwa lugha ya Kiswahili, ungetarajia kuwa Varwa wangesahau na kuacha kabisa mila na desturi zao. Hata hivyo, hali haiko hivyo. Varwa hutunza na kuzingatia mila na utamaduni wao moja kwa moja licha ya kupitia kwenye kipindi cha mabadiliko mengi. Mwanzoni baadhi ya Varwa walishawishika kufuata mila na desturi za Kimasai ambazo ndizo zilizokuwa zimetawala eneo lote karibu na Varwa, pamoja na zile za Waarusha walio Wamasai wanaopendelea kulima ambao tokea mwaka 1830 walihamia na kuishi eneo la Arusha, wakawa majirani na Varwa kwa upande wa kusini-magharibi mwa Mlima Meru. Hata hivyo, Varwa kwa ujumla waliendelea kushikamana na kuzingatia mila zao.[10] Kwa wakati huu, wanao mfumo wa maisha na utawala wa aina yao wenyewe. Wamegawanyika kwenye koo mbalimbali kwa kufuata utawala wa kuumeni. Wajibu mkubwa wa koo ni kusimamia shughuli za ardhi na taratibu za marika mbalimbali ambayo, kadri miaka inavyopita, yameanza kujijengea desturi zao tofauti na zile za Kimasai zilizoingia pale mwanzoni.

Kila kaya husimamia nyumba yake kiuchumi. Mashamba yanayoliwa na kaya kimsingi ni mali ya baba ambaye naye huwarithisha watoto wake wa kiume tu. Kijana wa kiume akishakua hujenga nyumba yake ndani ya shamba alilomegewa na baba yake, na majirani zake huwa ni wale ndugu zake. Kwa desturi, wanawake hawarithi mashamba wala hawana ng'ombe

[10] P.H. Gulliver, Social Control in an African Society. A Study of the Arusha: Agricultural Maasai of Northern Tanganyika (Routledge and Kegan Paul, London, 1963).

isipokuwa kuku tu. Wao hufanya kazi nyingi za shamba, na hawana shughuli sana na mambo ya kijamii nje ya familia zao, huu ni wajibu wa wanaume tu. Wachumba hawapaswi kuwa ndugu.au wale ambao ndugu zao wameshaolewa tayari kwenye familia ile.

Varwa wanazo koo 18 ambazo kimsingi zinazoundwa na ndugu wa kizazi kimoja kikihesabika kuumeni, na ambazo zimetapakaa eneo zima la Varwa zikiwa na tofauti ya idadi ya watu kwenye kila eneo. Kila ukoo huchagua kiongozi wake wa eneo au nyumba (mshili) na washili hawa wa nyumba mbalimbali huchagua mshili mkuu wa ukoo husika. Hawa washili wakuu toka kila ukoo nao huchagua mshili mkuu wa koo zote za Varwa. Kila ukoo unalo jukumu la kushughulikia mambo yote ya ardhi kama vile urithi na mipaka ya mashamba, na pia ni lazima ukoo utoe idhini ya uuzaji wa ardhi (shamba) kwa yeyote nje ya ukoo ule. Watu wa ukoo mmoja wana mshikamano wa hali na mali kwenye mambo mengi, kwa mfano, katika sherehe za harusi, vifo, na pia kwenye ulipaji wa fidia kwa mtu aliyeuawa ambapo wana ukoo wote huchangia sehemu ya gharama zinazohusika.

Idadi ya koo ni kama mara dufu ya ile ya marika ambayo hufuata mtindo unaofanana na ule wa Wamasai. Wanaume wote wamegawanyika kimarika kufuatana na umri wao, kila rika linalo jina lake na mshikamano ni mkubwa kati ya watu wa rika moja. Kwa kuingizwa jandoni vijana hujiunga kwenye rika ambalo lipo wakati huo, yaani huwa wa rika moja na vijana wenzao. Kila rika jipya litaendelea kuongezewa vijana wapya (*vasero* kwa Kirwa) wanaotahiriwa katika kipindi cha miaka ipatayo kumi na tano au zaidi kidogo. Baada ya muda huo vijana hawa hustaafishwa kwa sherehe kubwa na wakati huo huo kwenye sherehe hiyo husimikwa rika jipya la vijana na

kukabidhiwa silaha mbalimbali kama vile sime na fimbo, na huo unakuwa mwanzo wa rika jipya na wote wanaoingizwa jandoni wanahesabiwa kuwa wa rika hilo jipya. Kati ya wajibu muhimu katika rika jipya ni ulinzi wa jamii yao, ikilazimika hata kwenda vitani, kutafuta na kurudisha ng'ombe walioibiwa, hasa na Wamasai (jambo ambalo lipo bado katika maeneo ya wafugaji). Wajibu mmojawapo wa rika kubwa, la wazee, ni kutoa ushauri. Kwa ujumla ni kwamba, kama wasimuliavyo Varwa wenyewe, mtindo wa marika una umuhimu na jukumu kubwa kwa jamii, kama kuhakikisha kuwa kila mtu anakuwa na heshima na utii kwa wazee. Mkazo wa utii na uadilifu, ambao hufundishwa kwa siri pamoja na mambo mengine kwa vijana wanapoingizwa jandoni, unapaswa kuzingatiwa na kila mmoja katika rika lake. Kila rika kwenye eneo lao huchagua kiongozi (mshili) wao. Baadaye washili hawa wa maeneo huchagua mshili kiongozi ambaye himaya yake ni kwa Varwa wote kwenye rika husika.

Varwa huongozwa na kingozi mkuu, mshili mkuu *(nshili nnini)* ambaye huchaguliwa na washili wote pamoja na wazee ambao hukutana chini ya mti maalum wa *Mringaringa*, ambao kwa kitaalam huitwa *Cordia abyssinica* uliopo eneo liitwalo Poli lililo katikati ya kwa-Varwa. Mshili mkuu, akishachaguliwa anawakilisha na kuwa na mamlaka juu ya Varwa wote. Mtindo huu wa mshili mkuu ni mpya ambapo mshili mkuu wa kwanza wa namna hii alichaguliwa mwaka 1951. Mwanzoni uongozi huo uliwekwa na wakoloni kufuata mtindo wa u-*mangi*, ambapo Varwa waliwaona *mangi* hawa kutawala kwa manufaa ya wakoloni zaidi, hasa katika wajibu wao wa kusimamia ulipaji wa kodi, hivyo watu hawakupendezwa nao sana. Mnamo mwaka 1963 *Mangi* wa kumi na sita, na wa mwisho, alishuhudia nafasi hii ikifutiliwa mbali na Serikali ya Tanzania.

Hatua hii ya Serikali hata hivyo haikuweza kufuta heshima na wajibu wa Mshili Mkuu, yeye hufanya kazi zake licha ya kuwa hatambuliki rasmi na Serikali.

Mzozo huu wa kwa-Varwa ambao tutauelezea sasa lilikuwa tukio lililopima mshikamano wa makundi mbalimbali ya jamii ya Varwa, jukumu na ushawishi wa mshili mkuu, pamoja na hatua za taasisi nyingine za utawala na mamlaka ndani ya kanisa na toka serikalini.

## MZOZO WENYEWE

Kati ya sababu nyingi zilizoibua mzozo huu wa kidini ambao uligusa maisha ya jamii nzima ya Varwa kuanzia mwaka 1990 - 1993, baadhi zilikuwa na msingi wa siku nyingi, na nyingine ni hali fulani iliyojitokeza tu wakati huo huo. Kuna hisia kuwa kishawishi kikubwa kwa Varwa wengi kuingia kwenye mzozo huu ni uhamasishaji uliofanywa awali na viongozi wao wa kanisa ambao hata hivyo hawakubaliani na madai hayo. Hebu tuangalie hoja hii ya kwanza.

Varwa wanasema sababu ya kwanza iliyosababisha kutokea kwa mzozo huu wa kidini ni Wachagga katika Dayosisi ya Kaskazini kutotenda mambo kwa usawa kwa Varwa ambao ni wachache katika Dayosisis hii. Kuna ukweli kwamba Wachagga wanao utajiri mkubwa kuliko Varwa, na mali za Kanisa la Kilutheri zilizopo Uchaggani ni nyingi, bora na za kisasa na zenye uangalizi bora zaidi kuliko ilivyo kwa Varwa. Katika madai hayo, Varwa walitoa mifano ya idadi ya shule za sekondari na hospitali zilizopo Uchaggani kuwa ni nyingi sana na zenye majengo mazuri, bora na ya kisasa, kama vile hospitali ya Machame, Marangu na zingine huko Moshi, hali ambayo hailingani kabisa na ile ya kimaskini ya hospitali moja tu kwa Varwa iliyopo Nkoaranga.

Siyo kitu cha kushangaza kuona kuwa kuna tofauti kubwa ya kiuchumi kati ya Wachaga na Varwa inayojidhihirisha wazi kwa kuangalia tu mali na miundombinu ya kanisa iliyopo Uchaggani kulinganisha na ile iliyopo kwa Varwa. Uduni wa kiuchumi wa Varwa mbele ya Wachagga siyo jambo pekee tu linalozingatiwa hapa. Inasemekana wazi kuwa kulikuwa na hali ya kibaguzi kwa viongozi wa Dayosisi ya Kaskazini ingawa viongozi hao wanakanusha kabisa dai hili. Kuna baadhi ya taarifa

toka kwa wachunguzi wa nje kuwa viongozi wa Kichagga wa Dayosisi ya Kaskazini walikuwa na ukabila na walionyesha upendeleo wa wazi kwa Wachagga wa Dayosisi dhidi ya Varwa. Ndipo Varwa baada ya kuona kuwa fedha na nguvu zao walizotoa Kanisani zilitumika zaidi kwa manufaa ya Wachagga, waliamua kujitenga ili wafaidike na jasho lao. Hata hivyo, hatuwezi kuwalaumu Varwa kuwa walikuwa na ukabila kwa sababu zifuatazo: Kwanza, mzozo huu ulikuwa kwenye eneo la Varwa tu na pia uliwahusu Varwa peke yao, yaani kundi lililotaka kujitenga likipingana na kundi lililowatii viongozi wa kanisa. Wachagga hawakujumuishwa kwenye mapambano hayo. Tena, miongoni mwa watu kwenye kundi lililotaka kujitenga alikuwemo Mchungaji Bumija Mshana ambaye ni Mpare. Ni yeye huyu, na sio Nrwa, aliyewalaumu viongozi wa Kichaga katika Dayosisi ya Kaskazini kwa upendeleo wa ukabila. Kwa hali hii, je, mzozo huu ulisababishwa na ukabila wa kundi lipi? Hili ni swali gumu kujibu; jambo moja dhairi ni tofauti ya utajiri na hali ya maisha iliyo wazi kati ya Wachagga na Varwa. Iwe imetokana na ukabila au laa, tofauti hii yenyewe yaweza ikawa sababu mojawapo ya kutosha kuanzisha mzozo huu. Hali hii yafanana na vile vita vilivyotokea kule Cameroon kwenye Dayosisi Kuu ya Doula, kama wanavyoeleza waandishi Bayart na Mbembe, kuwa japo mzozo waweza ukaitwa ni ukabila kumbe ndani yake unaficha jambo.[11]

Sababu nyingine, iliyosababishwa na hali iliyojitokeza tu na kuchochea mfarakano uliopelekea mzozo huu, ilikuwa ni uchaguzi wa Askofu mpya wa Dayosisi ya Kaskazini mwaka 1976 kufuatia kifo cha Askofu aliyemtangulia. Ukali wa Askofu huyo mpya, Erasto Kweka, ambaye pia ni Mchagga kama yule

---

[11] "J. Bayart and A. Mbembe, 'La bataillc de 1'archidiocese de Douala', *Polilque Africaine* 35, *L'argent de Dleu* (1989), uk. 79.

aliyemtangulia, uliharibu uhusiano mzuri uliokuwepo baina ya Askofu na Varwa, uhusiano ambao tabia ya upole ya Askofu wa awali iliudumisha sana. Muda si mrefu baada ya Askofu huyu mpya kuwekwa wakfu alitamka maneno ambayo yaliwaudhi sana Varwa. Hii ilitokea wakati wazee wa Kirwa walipokwenda kwake kumlalamikia kuwa Dayosisi inawapeleka wanafunzi wachache sana wa Kirwa masomoni Ulaya kulinganisha na wale wa Kichagga. Askofu Kweka aliwajibu, "Wanaokwenda Ulaya wanaenda kwa vichwa vyao," akimaanisha kuwa "tunawachagua na kuwapeleka wenye akili tu." Tokea hapo, Varwa wakaamua kutafuta maendeleo yao kwa njia zao wenyewe. Varwa, ambao mpaka wakati huo walikuwa na shule moja tu ya sekondari ya Makumira, waliamua kuanza ujenzi wa shule nyingine mpya za sekondari. Mwaka wa 1987, shule ya sekondari ya Nkoaranga ilianzishwa, na mwaka uliofuata wa 1988 shule ya sekondari ya Engare Nanyuki ilianzishwa. Fedha zilizotumika kufungulia shule hizi zilichangwa na wanaviijiji husika na kwa msaada wa Kanisa.

Pale Nkoaranga, ujenzi wa shule ya sekondari ulileta mgongano na Askofu. Mnamo mwaka 1987 masomo yalianza chini ya mti. Mwaka wa 1990 viongozi wa Usharika waliamua kujenga madarasa ya shule kwenye shamba la kahawa ya kanisa la Kilutheri. Kahawa ziling'olewa bila idhini ya Askofu. Ndipo baadaye Askofu alipoombwa kusajili shule, lakini alikataa kusajili shule hiyo chini ya kanisa. Kwa mara nyingine tukio hili lilidhihirisha ugumu wa Askofu, hivyo kuzidi tu kuchochea mvutano.

Kwa upande mwingine, ujenzi wa shule hii ya sekondari ya Nkoaranga uliibua swali muhimu: Je mali za kanisa ni za nani hasa? Ikiwa wakati wa amani swali kama hili halipewi uzito wa haja, hali itakuwaje pale waumini wanapojitenga na

viongozi wa Kanisa? Nani hasa anayemiliki makanisa, mashamba, shule na hospitali? Hili ni swali zito kwani mali za Kanisa la Kilutheri kwa-Varwa ni nyingi na huduma yake inagusa jamii yote. Ukifikiria majengo makubwa na ya kisasa ya kanisa yaliyogharimu fedha nyingi, yamejengwa miongoni mwa watu na ni kama mhimili wa maisha ya kijamiii, na hivyo si rahisi kuyahamisha. Yapo kwenye ukanda huu wa kilimo ambapo ardhi ni adimu na ghali mno. Kama ni kujenga makanisa mapya, pesa na ardhi zitapatikana wapi? Hivyo basi, suala zima la umilikaji wa mali za Kanisa hili la Kilutheri ni mojawapo ya sababu kubwa zilizoibua mgongano. Watu walipigania haki ya kumiliki makanisa yao na kuabudia huko, haki ambayo viongozi wa juu wa kanisa lao waliipuuza.

Hali ya matatizo kama hayo haikuzingatiwa kabisa na viongozi wa juu wa Kanisa la Kilutheri ambao pia walipinga kabisa dai la Varwa kuwa hawapatiwi huduma kwa njia ya usawa. ilivyopaswa. Kanisa la Kilutheri liliweka msimamo wake kwenye taarifa yenye kurasa arobaini iliyochapishwa mwaka 1992. Sehemu ya taarifa hiyo ilichapishwa kwenye gazeti la *Business Times*.[12] Kufuatana na taarifa hiyo, viongozi wa kanisa hili waliweka bayana kuwa anayewajibika na mzozo huu ni Jackson Kaaya akiwa kiongozi wa mapinduzi hayo, na ambaye pia walimweleza kuwa alikuwa na uchu na kiu ya madaraka.

Huyu mtu ni nani? Akiwa na zaidi ya miaka sabini wakati wa mzozo huu, alikuwa mtu maarufu sana kwa Varwa tangu awali. Umaarufu wake hasa ulianza toka wakati wa mzozo mkubwa wa ardhi ya Wameru (Varwa) kwenye miaka ya 1950. Varwa walipambana na Serikali ya kikoloni ya

[12] *Business Times,* 25 December 1992.

Kiingereza wakipinga uporaji wa ardhi yao uliofanywa na wazungu katika eneo lenye rutuba na zuri kwa ufugaji huko Engare Nanyuki mashariki mwa Mlima Meru. Varwa waliyafikisha malalamiko yao juu ya uvamizi huo mbele ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNO) kwa kumtuma mwakilishi toka miongoni mwao, aliyeitwa Krilo Japheti.[13] Krilo Japheti na Jackson Kaaya wakiwa kwenye umri wa miaka thelathini hivi wakati ule, walikuwa ni miongoni mwa viongozi shupavu wa upinzani huo dhidi ya uvamizi wa kikoloni, na hivyo Varwa hujivunia sana juu yao. Mzozo huu wa ardhi ya Varwa ulikuwa mojawapo ya vichocheo vya kuanzishwa kwa chama cha siasa cha Tanganyika African National Union (T.A.N.U.) hapo 1954, chini ya uongozi wa Julius Nyerere, na pia chimbuko la kupigania uhuru wa nchi hii.

Jackson Kaaya, ambaye alikuwa mjoli wa Julius Nyerere, kwa muda mrefu alikuwa msimamizi wa vita dhidi ya rushwa akiwa mjumbe wa kamati ya halmashauri kuu ya CCM. Pia alikuwa mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Arusha, kiti alichokipoteza katika uchaguzi mkuu wa Chama hicho mwaka 1987. Kwa mujibu wa madai ya viongozi wa kanisa la Kilutheri, kupoteza kiti huko kwa Kaaya kulimfanya awe na uchu wa kupata tena madaraka, hivyo akaanza kutafuta mwanya huo mahali pengine. Alijipatia nafasi hiyo kwenye Kanisa la Kilutheri mwaka 1988 alipochaguliwa kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Dayosisi ya Kaskazini kwa kipindi cha miaka mine, na pia kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Jimbo la Meru katika Dayosisi hiyo. Kaaya akawa tena mtu maarufu wa ngazi ya juu akifurahia kupata nafasi hizo ndani ya Kanisa lake la Kilutheri.

[13] Kirilo Japhet and Earl Scaton, *^1'iie Meru Land case'* (East African Publishing House, Nairobi, 1967).

Mwaka 1989 Kaaya, alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Elimu na Maendeleo Meru (Meru Education and Social Development Trust - MESODET), chama kilichoanzishwa kwa juhudi za Varwa wote ili kusimamia matumizi ya fedha za maendeleo zilizochangwa na kila kaya ya kwa-Varwa. Hapo mwaka 1990, ilikubaliwa na Varwa chini ya MESODET kuwa kila kilo moja ya kahawa ikatwe shilingi za ki-Tanzania 1.25/= baada ya kuuzwa katika chama cha ushirika, mahali ambapo wakulima wote huuzia kahawa yao. Kiwango hiki cha makato hakikuwa kikubwa sana kwani kwenye msimu huo kahawa iliuzwa kwa shilingi 230/= kwa kilo moja katika vyama vya ushirika (ingawaje baadaye bei ya soko ilianguka sana). Shilingi milioni hamsini (50,000,0007/=) zilikusanywa na zilitumika kwa ujenzi na uendelezaji wa shule za sekondari, ufundi na pia hospitali ya Nkoaranga.

Kuanzishwa kwa MESODET kulidhihirisha maendeleo mazuri ya utawala na mshikamano wa uongozi wa Varwa, pia kulidhihirisha wazi utayari wake katika kujiletea maendeleo bila ya misaada ya kifedha kutoka Kanisani. Hata hivyo katiba anzilishi ya MESODET iliweka kifungu kilicholipa Kanisa la Kilutheri mamlaka ya kusimamia fedha za MESODET kama vile lilivyokuwa tayari likisimamia shule za sekondari, vyuo vya ufundi na hospitali zilizoko kwa Varwa. Kwa hiyo, Kanisa la Kilutheri lilihusishwa moja kwa moja na uanzilishi wa taasisi hii mpya ya MESODET na lilisimamia miundombinu ya kiutawala kwenye miradi yote bila ya kutoa fedha. Kwa ujumla kazi za MESODET ni za kukamilisha na wala siyo kushindana na shughuli zilizokuwa zikifanywa na Kanisa, japo kwa mtazamo wa Varwa kazi zake zilikuwa kuondoa mapungufu

yaliyojitokeza katika kuleta maendeleo ambayo ni moja kati ya malengo yaliyokuwa yamekusudiwa na Kanisa.

Hapo mwaka 1990 matukio mawili yalifanya Kanisa kupingana na Jackson Kaaya. Tukio la kwanza lilkuwa ni ule ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nkoaranga kwenye shamba la kahawa la kanisa. Jackson Kaaya, <u>akiwa mtu maarufu na aliyejulikana kwa siku nyingi katika usharika huu</u>, alichaguliwa na wazazi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hii akiwa na wajibu wa kuona kuwa shule inaendeshwa ipasavyo, na pia kuitisha mikutano kila inapolazimu. Kwa mtazamo wa viongozi wa Kanisa, ilionekana wazi kuwa Kaaya ndiye aliyechochea ung'oaji wa miche hiyo ya kahawa katika shamba la kanisa. Tukio la pili, katika mwaka huo huo, lilikuwa la mtazamo wa kiroho zaidi na lilisababisha kuvunjika kwa uhusiano mzuri kati ya Kaaya na Askofu. Kwenye sherehe ya harusi ya kijana wake, Kaaya aliwapa pombe wageni wake jinsi tu ilivyo kawaida ya utamaduni wa Varwa. Kanisa la Kilutheri linalaani unywaji wa pombe na limekuwa likipambana nayo kwa nguvu na kwa muda mrefu hapa kwa-Varwa. Varwa, kama walivyo Wachagga, licha ya mafundisho ya kanisa bado huendelea kuwa wanywaji sugu wa pombe hasa ya mbege ambayo hulevya kwa haraka sana. Kwa siku za nyuma, unywaji wa pombe ulikuwa jambo la kawaida sana hasa kwa wazee wakati wa mchana na hata sasa baadhi yao wanaendelea kufanya hivyo. Kuwapa watu idadi fulani ya madebe ya pombe ni jambo la lazima na la msingi kwa Varwa pale mtu anapotaka kuwakutanisha wazee pamoja, pengine katika shauri fulani kama shauri la ugomvi wa shamba, au kutoa mahari, au shauri la mauaji. Pombe ya mbege ambayo ilikuwa ikinyweka kwa wingi katika sherehe mbalimbali na hasa zile za harusi, kwa sasa inaelekea kurithiwa na pombe ya

chupa kama bia na zaidi sana soda, hii ikiwa ni kutokana na msisitizo wa kimaadili wa Kanisa la Kilutheri.

Kanisa lilimwadhibu vikali Kaaya, walimwondoa katika nafasi yake ya kuwa mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Dayosisi na pia kama mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Jimbo la Meru katika Dayosisi hiyo. Inavyoonekana ni kuwa Kaaya alipewa adhabu hii kali sio tu kwa kuvunja maadili ya kiroho, bali pia kutimiza nia ya kumwadhibu kutokana na baadhi ya matukukio ya nyuma. Kwa Kanisa kufanya jambo hili la adhabu kama uonevu kulimsababisha Kaaya kuwa na mtizamo wa kujitenga, na siyo yeye peke yake tu bali pia jamii kubwa ya Varwa ambao Kaaya alikuwa mwakilishi wao. Varwa wengi waliona adhabu dhidi ya Kaaya kama mfano mwingine wa kitendo cha uonevu toka uongozi wa Kanisa. Watu waliuliza, ni kwa nini Kaaya aadhibiwe kiasi hicho wakati ambapo Wachagga hunywa pombe namna iyo hiyo ila wao hawaadhibiwi?

Hisia za maonevu kama hayo ndizo zilikuwa kichocheo kikubwa cha Varwa kufikia azma ya kutaka kujitenga. Hamasa za watu zilipamba moto kwa haraka. Katika mkutano wa hadhara hapo tarehe 29 Septemba 1990 (mwenyekiti wake akiwa Jackson Kaaya) viongozi wa MESODET waliilaumu Dayosisi ya Kaskazini kwa kutaka kwa makusudi kurudisha nyuma maendeleo ya Jimbo la Meru. Tarehe 3 Oktoba 1990 viongozi wanne wa ngazi ya juu wa MESODET waliamua kuitisha mkutano wa hadhara kujadili kuanzishwa kwa Dayosisi yao mpya ndani ya Kanisa la Kilutheri, itakayoitwa Dayosisi ya Mlima Meru. Walimwomba Mchungaji Mkuu wa Jimbo la Meru ashiriki na aitishe mkutano huo, lakini alikataa. Hata hivyo mkutano huo uliitishwa tarehe 29 Oktoba 1990 na ulihudhuriwa na watu 77 chini ya uenyekiti wa Kaaya. Mkutano huo ulipitisha azimio la kuanzishwa kwa dayosisi hiyo mpya itakayozinduliwa

tarehe 1 Januari 1991. Ombi la usajili wa dayosisi mpya lilitumwa kwa haraka Serikalini na hatimaye tarehe 15 Desemba 1990 Dayosisi hiyo mpya ilisajiliwa.

Kanisa la Kilutheri likaanza kwa haraka kupinga usajili wa Dayosisi hiyo mpya kwa njia za kiufundi na likafaulu kushawishi kufutwa kwa usajili huo tarehe 16 Februari 1991. Pia lilifanikiwa katika mahakama ya Arusha kupata hati ya kuzuia Dayosisi hiyo mpya kutumia jina la Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, kwa kifupi KKKT. Hata hivyo wana Dayosisi hii mpya waliendelea kutumia vifupi hivyo vya KKKT kwani walijihesabu kuwa wao ni Walutheri na tena ni waumini wa Kanisa hilo. Zaidi ya hilo, waliamua kuendelea kusalia kwenye makanisa hayo ya Kilutheri katika eneo lote la Varwa. Tokea hapo basi malumbano makubwa yaliendelea katika eneo la Varwa katika kushawishi waumini kujiunga na upande wao kwa wingi iwezekanavyo. Hali ikawa ya wasiwasi na ya hatari, pia vurumai zilizuka mara kwa mara kati ya wale waliojitenga na wale wengine hasa kwenye milango ya makanisa, ukiwepo pia uharibifu wa mashamba na mali za kanisa. Serikali iliagiza pawe na utulivu na amani na sheria zifuatwe.

Uasi ulizidi kuenea kila sehemu, na mwaka mmoja tu baadaye Kanisa la Kilutheri lilijikuta likilazimika kuunda Dayosisi katika Jimbo la Meru. Tarehe 11 Machi 1992, wajumbe wa Halmashauri Kuu ya KKKT walipiga kura kupitisha uundwaji wa dayosisi mpya ya Meru ambayo ilikuwa ya kumi na tisa katika dayosisi za KKKT, pia Askofu aliteuliwa. Kwa kufanya hivyo, Kanisa la Kilutheri lilitumaini lingeanzisha kwa upya uhusiano na himaya yake kwa-Varwa. Lakini uamuzi huu ambao ulikuja kwa kuchelewa mno, ulipingwa vikali na wapinzani waanzilishi wa Dayosisi ya Mlima Meru, (tofautisha Dayosisi ya Mlima Meru na Dayosisi ya Meru iliyoundwa na Kanisa), ambao walilitaka Kanisa liitambue

Dayosisi ile yao ya Mlima Meru. Waliamua kupinga kwa uwezo na nguvu zao zote uundwaji wa dayosisi nyingine yoyote nje ya ile yao.

Kuzaliwa kwa Dayosisi ya Meru kuliongeza kasi ya ghasia na vurugu zaidi. Tarehe 18 Machi 1992 wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanisa la Kilutheri wapatao 710 walikutana kwenye Kituo cha Mafunzo kwa wenye Ulemavu Usa River kwa madhumuni ya kupitisha Katiba ya Dayosisi yao mpya na kudhibitisha uteuzi wa Askofu na watumishi waandamizi. Lakini wakereketwa wa Dayosisi pinzani walikuwa wameapa kuuvuruga mkutano huo. Waandamanaji wapatao elfu moja na mia tano walilizingira jengo hilo wakiwa wamebeba mawe, mishale, mikuki, marungu na mapanga. Walijaribu kuingia ndani ya jengo hilo kwa nguvu ili kuwaona Maaskofu. Kikosi cha polisi wa kuzuia ghasia kiliitwa mara moja. Ilichukua muda wa masaa mawili kuwatawanya waandamanaji hao. Askofu mmoja alijeruhiwa, magari kumi na nne yaliharibiwa, na mpinzani mmoja aliuawa kwenye mapambano hayo.

Siku na majuma yaliyofuata, mapambano yaliyoanzia Nkoaranga yalienea na kuzidi kukua. Mtafaruku huu pole pole ulienea eneo zima la Varwa. Ni eneo la Engare Nanyuki tu lililoko upande wa mashariki ndilo ambalo halikupatwa na machafuko hayo. Tarehe 25 Machi 1992, kule Sakila polisi walifukua maiti ya mtu mwanaume aliyekuwa ameuawa kwa kukatwakatwa kwa mapanga na kuzikwa harakaharaka kwa siri. Siku iliyofuata, nyumba 23 ziliharibiwa vibaya kule Nkoaranga, Seela na Sing'isi, na pia watu watatu zaidi waliuawa. Nyumba ziliendelea kuchomwa hasa nyakati za usiku na morani huku wakiimba nyimbo za kiasili za kuashiria vita zenye asili ya mori wa Kimasai, kuonyesha kama uasi nyakati za zamani. Mwezi Aprili hali ya wasiwasi ilitanda kote Poli na King'ori, yakiwa ndiyo maeneo ambapo mzozo huu ulikuwa mkubwa zaidi. Kilele cha vurugu

kilifikiwa mwezi Aprili na Mei ambapo familia sitini zilipopoteza makazi yao yaliyochomwa moto, pia watu watano waliuawa na mali nyingi ziliteketezwa zenye thamani iliyokadiriwa kufikia shilingi za Tanzania milioni sabini na tatu. Wale walioathirika vibaya na mkasa huu walikwenda kuwaona viongozi wa Mkoa mjini Arusha ili kulalamika na pia kutafuta misaada.

Mwishoni mwa mwezi Aprili 1992, ujumbe wa wakimbizi hao ulikwenda Dar-es-Salaam kuomba kuonana na Rais wa Jamhuri ambapo walipokelewa na Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Edward Lowasa. Huyu aliwapokea na baada ya mazungumzo nao, kwa moyo mkunjufu aliwatakia safari njema kurudi nyumbani. Ndipo wakaamua kuarifu vyombo vya habari.[14] Kwa upande wao vingozi waKanisa la Kilutheri waliamini kwamba wameshatekeleza wajibu wao katika kutatua mzozo huu, hivyo wakaomba Serikali kuingilia kati. Mwanzoni mwa mwezi Mei 1992 maaskofu wa K.K.K.T walipokelewa na Rais Mwinyi. Kunako tarehe 27 Mei, katika kujaribu kutafuta suluhisho la amani, Rais alipokea pia ujumbe wa watu kumi na moja kutoka upande wa upinzani. Baada ya mkutano huo, Halmashauri Kuu ya Dayosisi pinzani iliitisha kikao cha dharura na kuamua kutangaza na kuhubiri amani kwa Jumapili tatu mfululizo. Hata hivyo tumaini la kuwepo kwa amani lilikuwa dogo hasa kwa vile Kaaya alishatamka dhahiri kuwa "Haitakuwepo amani endapo hatutapewa haki ya kuwa na Dayosisi yetu wenyewe."[15] Msimamo huu ulikuwa na nguvu mno, hasa kutokana na idadi kubwa ya sharika zilizounga mkono kundi lake ambazo zilikuwa thelathini na moja kati ya thelathini na tano za Jimbo hili la Meru.

---

[14] *The Express*, 23 - 29 April 1992.
[15] *Daily News,* 3 June 1992.

Kwa kutaka kuthibitisha hali halisi ilivyokuwa, Serikali ilituma ujumbe kufanya uchunguzi wa takwimu ya idadi ya wafuasi wa kila kundi. Ripoti yao ilionyesha kuwa viongozi wa Kanisa walikuwa watiifu kwa Askofu (kati ya wachungaji na mashemasi thelathini na tano na wainjilisti mia moja na kumi na nne wa Jimbo, ni wachungaji watatu tu na wainjilisti kumi na tano walijiunga na Dayosisi pinzani), na ambapo kwa jumla idadi kubwa ya waumini wote waliunga mkono Dayosisi pinzani. Hadi kufikia mwezi Juni 1992, makisio yalionyesha kuwa kati ya asilimia 80 hadi 95 ya Walutheri wa Jimbo la Varwa walikuwa wakiunga mkono Dayosisi pinzani ya Mlima Meru. Kwa uhakika hapakuweko na ulinganifu wo wote kati ya wachungaji na waumini (isipokuwa kwenye vijiji viwili tu, Sing'isi na Mulala, ambapo waumini karibu wote waliunga mkono Dayosisi ya Meru, ila wao hata kama ungewachanganya wote wasingefikia asilimia kumi ya waumini wote wa Jimbo hilo). Yaelekea safari ilifikia njia panda na mzozo ukachukua sura mpya ya kiitikadi.

Kwa kutokuwa na uwezo wa kujieleza kwa kutumia vyombo vya habari, magazeti na redio, ambavyo vilitawaliwa zaidi na Serikali pamoja na Kanisa, wapinzani walinadi sera zao kwa njia ya kutumia barua za wazi. Moja ya barua hizo iliandikwa hapo mwezi Mei 1992 ilipinga kabisa matumizi ya mabavu yaliyofanywa na ule upande mwingine, ilidai kuwa kanisa la Usa River lilitumika kama kituo cha mafunzo ya kijeshi na viongozi wa Kanisa, na wakati wa kwenda kuhubiri Askofu Kweka alisindikizwa na askari polisi (kwa mfano kule kanisani Ndoombo). Tabia hii, barua ilisisitiza, inapingana kabisa na uhuru na dhamiri ya mtu ambayo ni nguzo kuu katika masuala ya imani kama alivyofundisha Martin Luther mwenyewe. Wapinzani walijieleza kuwa wao ndio wafuasi

halisi wa imani ya Kilutheri na hivyo wanapinga kabisa utawala wa mabavu, uroho wa madaraka pamoja na ukoloni mamboleo uliofanywa na wachungaji, mambo ambayo, kama walivyodai, ndiyo yaliyopelekea kuwepo kwa matatizo yote. Pia walijieleza kwa njia ya mabango na michoro (ona mabango na michoro katika vielelezo).

Licha ya wito wa utulivu uliokwishatolewa, mvutano bado ulibaki kuwa mkali na hatima yake haikuonekana katika upeo wa karibu, na zaidi hasa kutokana na Serikali kuitambua Dayosisi mpya ya Meru iliyoundwa na kuungwa mkono na kanisa. Mwishoni mwa mwezi Mei vurugu na varumai kali zilitokea huko Nkoaranga na Makumira na hata kusababisha Serikali kwa mara nyingine kutuma vikosi vya askari huko. Viongozi wa Dayosisi ya Mlima Meru walilaani kitendo hiki cha kutumia askari ambacho walidai hakitaleta amani bali kilichochea moto wa mapambano zaidi. Waumini wa upande mwingine nao wakawatupia lawama viongozi wa Dayosisi ya Mlima Meru kwa kusababisha hali ambayo ililazirnisha matumizi ya nguvu za kiaskari kuingilia kati.

Wakati huo huo, Askofu wa Dayosisi ya Meru, Paulo Akyoo, aliwekwa wakfu tarehe 21 Juni 1992 chini ya ulinzi mkali wa askari. Ingawaje viongozi wa Serikali walialikwa katika sherehe hiyo, hata hivyo hawakudhuria kwani walioona kuwa kitendo cha kuwekwa wakfu kwa Askofu huyo kilienda kinyume na juhudi za Serikali katika kuleta upatanisho. Kutohudhuria sherehe hiyo kulidhihirisha msimamo wa Serikali kinyume na Kanisa katika jambo hilo. Pia Walutheri kwa Varwa waliokuwa upande wa Dayosisi ile inayoitwa ya waasi, walichukulia kitendo hicho kuwa ni cha kufifisha juhudi za usuluhishi. Ikiwa na lengo la kuridhisha pande zote mbili, Serikali ilitangaza tena usajili wa Dayosisi

ya Mlima Meru. Cheti cha usajili wa dayosisi hii kilitiwa sahihi na kiongozi wa Serikali tarehe 29 Juni 1992 kule Dar-cs-Salaam, na usajili rasmi ulifanywa tarehe 26 Julai 1992. Wakati huo huo, tarehe 24 Julai 1992, Serikali ilisajili Dayosisi ya Meru. Tokea hapo Dayosisi hizi mbili za Kilutheri zinazohasimiana zikawa zinatambuliwa rasmi na Serikali zikiwa katika eneo moja.

Miezi kadhaa iliyofuata, vita vikali vya kiitikadi na hasa katika magazeti vilitawala kati ya Dayosisi hizi mbili. Kwa bahati yake, Kanisa la Kilutheri kwa kujulikana kwenye vyombo vya habari, liliweza kuchapisha taarifa nyingi kwenye magazeti zenye kukashifu Dayosisi hasimu kama genge la wahuni wanaowalazimisha waumini wajiunge nao. Kwa kutokuwa na uwezo na ushawishi kwenye vyombo vya habari, Dayosisi pinzani ilikuwa ikijibu baadhi ya shutuma hizo kwa njia ya barua za wazi. Mojawapo ya barua hizo iliandikwa tarehe 6 Oktoba 1992 na Mchungaji Mshana ambaye ni Mpare, ambaye awali alikuwa mkufunzi katika Chuo cha Kilutheri cha Makumira kabla ya kufukuzwa kwake na Kanisa la Kilutheri mwanzoni mwa mzozo huo kwa kuwaunga mkono wapinzani. Barua hii iliandikwa kwa 'Senkali ipendayo amani' ikimwelezea Askofu Kweka kuwa ni mtu dhalimu anayetunga mambo na kutuma mawazo yake mwenyewe kwenye vyombo vya habari. Barua hiyo pia ilikemea na kupinga mwenendo wa Kipentekoste ulioingizwa ndani ya Kanisa la Kilutheri. Ni wazi kabisa kuwa Kanisa la Pentekoste lilikuwa linafaidika sana na matokeo ya mzozo huu wa kwa-Varwa kwani Walutheri wengi waliokatishwa tamaa na mapigano haya walikimbilia kwenye dhehebu hilo. Kanisa la Kipentekoste, lililoanzia kule Marekani mwaka 1906, lilifika hapa kwa Varwa mwaka 1968 katika kijiji cha Mulala, kaskazini mashariki mwa Nkoaranga, sehemu

ambayo Kanisa la Kibaptisti lilikuwa limeshaanzishwa takribani miaka miwili kabla ya hapo. Licha ya tofauti kubwa iliyopo ya kitheologia kuhusu ubatizo, pia Wapentekoste wanatofautiana na Walutheri kwa mkazo wao mkubwa wa kupinga ulevi na kuoa wake wengi (mambo ambayo lawama za barua ya Mshana zinahusika nayo kwa kiasi hapa).

Wapentekoste hujiona kuwa na maadili bora zaidi kuliko Walutheri na mihadhara ya kuhubiri kwao ni jambo la msingi sana. Hivyo, hata Wapentekoste wachache tu watosha kuwashawishi watu. Kwa vile Wabaptisti hawana mihadhara ya kuhubiri mithili ya Wapentekoste, wao sio tishio sana kwa Kanisa la Kilutheri. Ueneaji wa haraka wa Wapentekoste ulitishia viongozi wa Kanisa la Kilutheri na ili kukabiliana na hali hii walianzisha sera ya uamsho mwaka 1978 ndani ya Kanisa la Kilutheri iliyoanzia kule kule Mulala ikisisitiza maisha ya wokovu kwa kila mtu, amani na utulivu. Kutokana na hali hiyo ya kujiingiza kwa upentekoste ndani ya Kanisa la Kilutheri ambayo ililaumiwa na Mshana kwenye barua yake ya tarehe 6 Oktoba 1992, mzozo huu ulichukua sura mpya ya malumbano ya Kitheologia jambo ambalo halikuwepo mwanzoni, pengine kwa vile waanzilishi wa Dayosisi ya Mlima Meru hawakuwa watheologia zaidi ya Mshana.

Barua nyingine ya wazi kutoka Dayosisi ya Mlima Meru ni ile ya tarehe 30 Oktoba 1992 ya Mchungaji Baltazar Kaaya yenye maudhui kama hayo. Iliandikwa kwa viongozi wa Kanisa ikiwa ni jibu la tuhuma zilizokuwa zimeandikwa katika magazeti. Iliwaelezea wapinzani kuwa wao ndio Walutheri halisi na waliopinga kata kata ma-papa na ma-askofu kujiingiza kati ya Mungu na waumini wake. Katika barua hii, Baltazari Kaaya aliwaeleza viongozi wa K.K.K.T kuwa: "Wajibu wenu ni kuwahudumia Wakristo na sio kuwahukumu, tena hapa

ndipo mnapokosea kwa kutaka kuwanyang'anya waumini wa Dayosisi ya Mlima Meru uhuru wao wa kuabudu kwa kutaka kuilazimisha Serikali kufuta usajili wao...." Kwa kumalizia alisema: "Sisi ni watu huru wa Mungu na hakuna mtu yeyote anayeweza kuingilia kati kwenye dhamira na mahusiano yetu na Mungu."

Kanisa la Kilutheri lilizaliwa mwanzoni mwa karne ya kumi na sita kutokana na mzozo ambapo Wakristo walihoji mamlaka walijokuwa nayo wakuu wa Kanisa, sasa Kanisa hili la Kilutheri nalo hapa lilijikuta likiwa upande wa kulaumiwa. Hili likiwa jambo la kipekee kabisa hapa Afrika ya Mashariki. Swali hili la kuhoji mamlaka ya wachungaji lilizua maswali mengi baina ya Wakristo wengi kwa Varwa, sio tu miongoni mwa Walutheri wa pande hizi mbili bali pia kati ya Wapentekoste, Wabaptisti, na vikundi mbalimbali vya uamsho vilivyoanzishwa ndani ya Kanisa la Kilutheri kunzia kule Mulala mwaka 1978 katika jitihada za kupambana na wimbi la madhehebu. Lakini Kanisa la Kilutheri lilionekana kupuuzia malumbano kama haya, na badala yake lilichukua tu hatua ya kuitenga Dayosisi ya Mlima Meru.[16] Msimamo huo haukuzuia Kanisa hili kupoteza mamlaka yake ya kidini na ushawishi wa kiroho lililokuwa navyo hadi wakati huo.

Katika sakata hili la kiroho, Kanisa la Kilutheri lilionekana kukosa uelewa wa haraka kuhusu tuhuma dhidi yake, na badala yake likajaribu tu kugeuzia malumbano sehemu nyingine. Kwa mtazamo wake, Kanisa la Kilutheri liliwaona wapinzani kuwa ni wafuasi wa shetani, walevi na wenye kupendelea mitara kinyume na mafundisho ya Kanisa, na pia watu wanaotamani kurudi kwenye mila potofu za kizamani. Ni kweli kuwa madai ya

[16] Angalia barua ya Askofu Kolowa katika gazeti la KKKT la *Umoja*, 1 & 2, (1992) uk. 32.

kutunza baadhi ya mila yalipelekea upinzani utokee. Hisia za kikabila kama Varwa, ambazo ndizo kichochezi kikubwa cha mzozo huu, zilionekana kwanza katika madai ya "ukabila" ndani ya kanisa, tuhuma zilizotolewa na pande zote mbili na ambazo zilijenga msingi wa malumbano tangu pale mwanzo. Pili, ni kule kufukuzwa kwa Jackson Kaaya pamoja na wafuasi wake kulikotokana na tuhuma dhidi ya ulevi pale alipoweka pombe katika sherehe ya harusi ya mwanae wakati ambapo Kanisa lilishapiga marufuku pombe katika sherehe zote za kikanisa. Lakini zaidi ni vile vitendo vilivyofanywa na wapinzani vya kuwachomea nyumba wenzao vyenye sura na desturi za kale kama vile vilivyofanywa zamani (Serikali ya Kiingereza ilifanya vitendo vya aina hiyo kwa wenyeji kule Engare Nanyuki wakati ule wa mzozo wa ardhi ya Varwa). Mbinu hizi zilipangwa na vikundi vya vijana (*vasero*) waliokuwa wakikutana usiku huku wakiimba nyimbo za kuashiria vita zenye asili ya Kimasai kama ilivyokuwa nyakati za zamani. Vijana hawa wanaunda kundi moja la wajibu katika marika ya Varwa. Hata mapigano yaliyotokea katika mzozo huu yalifanywa kirika, yakiongozwa na rika hilo la vijana, wakionyesha wajibu wao wa kulinda nchi yao. Hata silaha zilizotumika ni za kijadi, mawe, sime, (kama Wamasai), mishale, rungu na mapanga; silaha zilizotumika zamani na zilizo kinyume na silaha za kisasa za jeshi la Tanzania. Yote haya yakionyesha nia ya kulinda msimamo wao kwenye mzozo ambao hauna uhusiano wowote na mambo ya kizamani ila tu kwamba wapinzani hawa wa Kirwa walishindwa kujinasua toka kwenye mfumo wa mila na jadi zao zilizowalea. Kwa kiasi kikubwa mwendo wa mzozo huu wafanana na maasi ya wakulima ambayo kwa vyovyote huishia kwenye kushindwa. Hapa haina maana kwamba wapinzani hawa walifurahia kuendesha mambo kwa kutumia njia za kizamani, la hasha.

Hata hivyo mbinu hizi za kijadi zilitoa mwanya kwa K.K.K.T kuwaelezea kama wanamila na hivyo basi kujigamba kwamba hayo yalikuwa mapambano kati ya taasisi ya kisasa (K.K.K.T) dhidi ya mila duni za kizamani.

Basi Kanisa hapa likatangaza kwa wazi kupinga kwake unywaji wa pombe na kuonyesha madhara yake, na pia ubovu wa kuwa na mitara. Ni kweli kuwa unywaji wa pombe ni jambo la utamaduni uliokuwepo miongoni mwa Varwa hata kabla ya kufika kwa Wamisionari wa Kilutheri mapema mwanzoni mwa karne ya ishirini. Lilikuwa jambo la kawaida kwa wazee kupumzika na kunywa pombe (*vari*) huku kinamama wakiendelea kufanya kazi mashambani. Pombe ilikuwa muhimu sana kwenye shughuli yoyote iliyohusu jamii. Kwa mfano, hakuna kikao cho chote cha ukoo ambacho hakikuwa na pombe na pia kwa jadi ulipaji wa gharama mbalimbali ulikuwa ni kwa mitungi ya pombe, kama vile kwenye shughuli za uchumba, mahari, na kulipa fidia kwa mtu aliyejeruhiwa. Kanisa lilikuwa likipingana na desturi za matumizi ya pombe na hata lilionekana kufanikiwa kwa sehemu kubwa. Hata hivyo desturi ya unywaji wa pombe haikupotea kabisa hasa miongoni mwa wanaume waliokutana kwenye vilabu vingi vya pombe kila siku nyakati za mchana kwa ajili ya unywaji.

Kuhusu mitara, Kanisa la Kilutheri lilipambana nayo tangu mwanzo na karibu lishinde jambo hili kwa njia ya ushawishi. Zamani wanaume walioa wake wengi ili walime mashamba, kwa kadri mtu alivyokuwa na shamba kubwa au mashamba mengi ndivyo alivyoshawishika kuoa wake wengi kwa ajili ya kulima mashamba hayo. Wanawake wenyewe walipendelea kuolewa mitara na walipinga sana Wamisionari walipotaka kuondoa utamaduni huo wa mitara. Hoja yao

ilikuwa kwamba mwanamke angekuwa na kazi nyigi sana kama angeolewa peke yake tu.[17] Ingawa kanisa lilipendelea ndoa ya mke mmoja bado liliacha uhuru kwa kiasi fulani; wale wenye wake wengi hawazuiwi kujiunga na kanisa na mara nyingi wanawake wao huwa ni wa kwanza kujiunga na kanisa na baadaye huwashawishi waume zao nao pia wajiunge na Ukristo. Tangu mwanzoni mwa karne hii, kuoa wanawake wengi kumepungua sana, sababu kubwa ikiwa ni kutokana na eneo la shamba kuzidi kuwa dogo zaidi na zaidi. Kwa kadri ya ongezeko la idadi ya watu, vijana wengi waliooana hawana eneo la ardhi la kuwatosha, jambo ambalo pia husababisha baadhi ya vijana hawa kuchelewa sana kuoa.

Ukiachilia mbali masuala ya pombe na mitara, Kanisa limekuwa likipambana na jambo lingine la utamaduni wa Varwa kufuataa mfumo wa marika kwenye jamii yao. Mfumo wa marika ndio unaotumika katika kusimamia nidhamu na utii kwa viongozi na wazee, lakini hata hivyo Kanisa limekuwa likiona kuwa mshikamano uliopo kati ya marika ni kizuizi cha watu kujiunga na Ukristo. Kanisa limekuwa likilaani vitendo vingine vinavyoambatana na sherehe za marika. Kwenye sherehe hizi za rika la zamani linapong'atuka na rika jipya kusimikwa, pombe hunyweka sana na ngoma za utamaduni huchezwa, mambo ambayo kanisa huona kuwa ni kuendekeza maovu. Kwa muda mrefu Kanisa limekuwa likipinga haya yote. Sasa matukio haya mapya ya rika la vijana kuchoma nyumba za waumini pamoja na kuwepo mshikamano wa marika mengine kinyume na ushawishi wa kanisa, kumechochea Kanisa kupinga kwa nguvu zaidi utamaduni na taratibu hizi za

[17] Thomas Spear (ed.) *Evangelisch-Lutherisches Missionsblatt. Extracts on Arusha and Meru,* 1897 - 1914, kimetafsiriwa ns C. M. Murphy (African Studies Program, University of Wisconsin-Madison, 1995), uk. 40.

marika. Iwe ni kutokana na upinzani wa Kanisa tu au la, kitu kilicho wazi ni kuwa wapinzani wa Kanisa la Kilutheri waliunga mkono utamaduni wa marika katika jamii yao kinyume na uongozi wao wa kanisa, na hivyo kuongezea zaidi mtengano uliokuwepo kati yao na wachungaji. Mtengano upo kwa wazi kuhusu unywaji wa pombe, kama utachukulia ule mfano wa Jackson Kaaya kuweka pombe kwenye harusi ya mwanae ambapo yeye mwenyewe hakuona ubaya wake. Hata hivyo, ni vema kuelewa kuwa siyo wote waliopinga kanisa hili wanaunga mkono suala la unywaji wa pombe. Kuhusu suala la mitara, inaonekana Kanisa linaendeleza tu msimamo wake, siyo kwamba jambo hili ni kero ya haja kwenye jamii kwani halipo sana siku hizi. Mwisho, utamaduni wa marika uliungwa mkono kwenye sherehe yake ya mwaka 1992 kwa kuwepo wachungaji wa Dayosisi pinzani.

Mwishoni mwa mwaka 1992, kwenye eneo la Engare Nanyuki, eneo ambalo halikukumbwa sana na mzozo huu, kulifanyika sherehe ya marika mawili, ambapo pia nilipata nafasi ya kuhudhuria. Katika sherehe hiyo, rika moja liling'atuka na jingine la vijana lilisimikwa. Sherehe hizi husherehekewa kuanzia ngazi ya vijiji au kata zikiandaliwa na rika linalong'atuka, na kwa kawaida sherehe hizi hufanyika kila baada ya miaka kumi na mitano. Sherehe iliyotangulia hii ilifanyika mwaka 1976. Katika hatua ya awali, sherehe ilifanywa na Kijiji cha Olukungw'ado peke yake, na hapa hapakuwa na mchungaji yeyote aliyehudhuria. Sherehe ya pili ilikuwa kubwa na ilijumuisha vijiji vinne vya Kata ya Engare Nanyuki, na ilihudhuriwa na wageni mashuhuri wakiwemo Mshili Mkuu, Moses Nnko, Kirilo Japhet ambaye ni shujaa wa ule mzozo wa Ardhi ya Varwa, na pia alikuwepo mchungaji mmoja wa Dayosisi pinzani. Mchungaji huyu alihubiri kwa

muda mrefu wakati wa sherehe hiyo bila kujali cho chote na alitumia nafasi hiyo ya sherehe ya jadi kufafanua mafundisho ya Kanisa.  Hivyo inaonekana wazi kuwa wafuasi wa Dayosisi pinzani hawakuona ubaya wowote kati ya dini wanayofuata na utamaduni unaofanywa katika jamii yao; bali haikuwa hivyo kwa wachungaji wa Kanisa la Kilutheri ambao wanajaribu kuoanisha mzozo kanisani kwa Varwa kuwa ni vita baina ya wana mila na ustaarabu wa kisasa na hivyo kujiona wao ni bingwa wa ustaarabu wa kisasa. Uhasama huu unaoletwa na kanisa kuhusiana na kuadhimishwa kwa mila katika jamii ya Varwa, na hasa katika sherehe za marika, unaweza kusababisha kuvunjika kwa utamaduni wa marika ambayo mpaka sasa ni nguzo muhimu sana katika mausiano ya kijamii kati ya mtu mmoja na mwingine.

Wakati Kanisa linajitahidi kupinga baadhi ya mila za Varwa, waumini wa Dayosisi ya Mlima Meru walikuwa wakipigana kuchukua umiliki wa zile taasisi zilizokuwa zikiendeshwa na Kanisa la Kilutheri Jimboni mwao. Wakati huo, baadhi ya wafuasi hawa walikamata gari la Mkuu wa Shule ya Ufundi ya Leguruki ambayo inathaminiwa sana kwa kufundisha vijana wa Kirwa ufundi stadi.  Kwa kuhofia kufungwa kwa Shule hiyo, walirudisha gari hilo, na Shule hiyo bado inaendelea. Hospitali ya Nkoaranga nayo ilitekwa, lakini kwa vile wapinzani hawakuwa na pesa za kulipa watumishi, waliiachia, na hivyo uendeshaji wa Hospitali hii ukawa umeadhirika mno. Kama ambavyo tumekwishaona, Dayosisi pinzani ilifaulu sana kuunganisha idadi kubwa ya Varwa. Iliungwa mkono na Mshili Mkuu, Moses Nnko, ambaye anaishi Kijiji cha Mulala sehemu ambayo waumini wake waliunga mkono Askofu wa KKKT. Katika hatua ya kuhimiza amani, Moses Nnko aliitisha mkutano wa adhara wa viongozi

wote wa Varwa huko kwenye *Mringaringa* mnamo tarehe 28 Desemba 1992. Mkutano huu haukufanikiwa kwani ni wafuasi wa Dayosisi pinzani tu waliohudhuria. Jambo hili lilimwangusha sana Mshili Mkuu kwa sababu wajibu wake mkuu ni upatanisho, na kwa kijadi pale anapoweka fimbo *(ndata)* yake katikati ya wagombanao kwa kawaida mara moja wanapaswa kuacha mapambano. Kwa vile upande mmoja wa wagombanao haukuhudhuria, matumaini ya amani kwa taratibu za kimila yalitoweka. Vivyo hivyo, kwa vile suluhisho halikupatikana, tegemeo la waumini wa Dayosisi pinzani la kumchagua Askofu pamoja na wasaidizi wake halikufanyika kwani Askofu huyo angetakiwa atambuliwa na Kanisa la Kilutheri. Kwa hali hiyo, Dayosisi ya Mlima Meru ambayo haikutambuliwa na Kanisa, ingawaje ilikuwa imetambuliwa na Serikali, haikuweza kabisa kutekeleza vyema wajibu wake inavyopasa. Familia nyingi ziliahirisha ubatizo wa watoto wao au harusi zao kutokana na mfarakano huu wa kidini, nia ikiwa ni ili kukwepa kufahamika ni wafuasi wa upande fulani. Uendeshaji wa shule nyingi uliadhirika mno, na maisha ya kawaida ya watu yakavurugika. Kwa kuhofia matatizo zaidi kutokea, Serikali ilipiga marufuku mikutano yote ya hadhara.

Wakiwa na nia ya kupata ufumbuzi wa mzozo huu, viongozi wa Dayosisi pinzani, licha ya kupigwa marufuku kwa mikutano yoyote, waliitisha mkutano pale Kilala tarehe 11 Februari 1993. Lakini mambo yalizidi kupamba moto na hata kuilazimu Serikali kuwasaka wale iliodai walikuwa wakieneza fujo. Serikali iliwaadhibu bila kujali ni wa upande upi. Wakati wa Pasaka ya mwaka ule vurugu ziliibuka tena. Siku ya Ijumaa Kuu, wafuasi wanne wa Dayosisi ya Mlima Meru walikamatwa kwa kuwazuia waumini wa upande mwingine kuingia

kanisani.[18] Kwenye Jumapili ya Pasaka mwaka huo huo wa 1993, katika eneo la Nguruma na Sing'isi waumini wa pande mbili walianza tena kupigana, kila upande ukiwazuia wapinzani wao kuingia Kanisani. Polisi waliingilia kati, lakini walikutana na zingiti la mawe.

Kwa kuwakamata wale viongozi wanne wa Dayosisi ya Mlima Meru katikati ya Mwezi Aprili, mzozo ulichukua sura mpya kwa sababu mbili: Kwanza, walilaumiwa kwa kukiuka agizo la Serikali la kutokuwepo kwa mkutano wowote; na pili, walilaumiwa kwa ubadhirifu wa fedha, Shilingi za Tanzania milioni kumi na mbili, zilizopotea toka mfuko wa MESODET.[19] Mara moja wale walioshitakiwa wakakanusha tuhuma zote dhidi yao; lakini Kanisa la Kilutheri liliafiki tuhuma hizo upesi na kudai kuwa hiyo ndiyo iliyokuwa sababu kubwa ya viongozi hawa kuanzisha mzozo huu na kudai kuwa viongozi wa Dayosisi ya Mlima Meru walikuwa wezi na ndiyo sababu walianzisha mtengano huu ili wapate kuficha madhambi yao kwa wafuasi wao wasio na mawaa.

Je, kashfa hii iliweza kuotesha mbegu ya mashaka miongoni mwa waumini? La, hasha; wengi wao waliona huo ulikuwa udhalilishaji mwingine; na mara tu baada ya kutangazwa kukamatwa kwa viongozi wao katikati ya Aprili 1993, waumini wa Dayosisi ya Mlima Meru waliitisha mikutano sehemu kadhaa (Akeri, Nkoanrua, Ambureni, Ndoombo na Seela) ili kuanza kupanga mikakati ya kukabiliana na wapinzani wao na pia kutafuta njia za kuachiliwa kwa viongozi wao toka gerezani. Matukio kadhaa yaliendelea kutokea hapa na pale, huku Dayosisi ya Mlima Meru, (ikiongozwa na mjoli wa siku nyingi wa Julius Nyerere, na hivyo kufaidi uungwaji mkono na

[18] *Uhuru* (Gazeti la Chama cha Mapinduzi, CCM), 9 April 1993.
[19] *Uhuru*, 15 April 1993.

Serikali pale mwanzoni), ilizidi kupata upinzani mkubwa. Tarehe 20 Juni 1993, nyumba ya muumini mmoja wa Dayosisi inayotambuliwa na Kanisa ilichomwa moto kule Ndoombo. Kila mtu alianza kuwa macho, na baadhi ya vijiji vilianzisha ulinzi wa usiku ili kujikinga na mashambulizi. Hili ndilo lililofanyika kule Sing'isi ambako karibu waumini wote waliambatana na upande wa wachungaji huku wakiwa wamezungukwa pande na wafuasi wa Dayosisi pinzani.

Juhudi za Serikali za kutuliza fujo na kusimamia amani ziliifanya Serikali ichukiwe zaidi na zaidi. Baadhi ya wenyeviti wa C.C.M wa vijiji walioonekana kuruhusu machafuko vijijini mwao walikamatwa na kuwekwa rumande kwa siku kadhaa. Katika kupinga hatua hizo, baadhi yao inasemekana walirudisha kadi zao za uanachama baada ya kutoka rumande, na wakaacha kwenda ofisini mwao huko vijijini kufanya kazi zao za utawala. Ni makatibu wa matawi tu waliendelea kufanya kazi, na hivyo huduma zikafifia mno. Wakiwa wameumizwa sana na kile walichoita ukandamizaji wa Serikali, Varwa wengi walionyesha chuki kwa Serikali yao na hata wakagoma kushiriki mambo mengi ya umma. Waligoma kabisa kulipa kodi. Upinzani na kutoridhika kukawa dhahiri kabisa na hata matukio ya ujambazi yaliyosukumwa na hali ngumu ya uchumi yakaanza kujitokeza kati ya vikundi vya vijana wakifurahia hali hii ya mzozo. Kwa Dayosisi ya Mlima Meru kutokuwa na uwezo tena wa kuthibiti vurugu hizo ilizozianzisha ikawa imepoteza heshima yake kwa kiasi kikubwa.  Kutokana na hali ya wasiwasi iliyokuwa imefikiwa, na kutokana na shinikizo na makanisa, Serikali ililazimika kufuta usajili wa Dayosisi ya Mlima Meru. Dayosisi hii ikawa imepokonywa kabisa uhalali wake wote.

Jackson Kaaya, akiwa kiongozi wa jahazi la upinzani, akawa mtu asiyetakiwa, na hivyo alikamatwa tena tarehe 28 Juni 1993, na ilipigwa marufuku ya mkusanyiko wa watu zaidi ya watano. Tarehe 7 na 8 Julai 1993, waumini wa Dayosisi iliyofutwa waliharibu nyumba na mabanda ya ng'ombe pamoja na mashamba ya wafuasi wawili wa Dayosisi ile nyingine ikiwa ni katika kulipiza kisasi. Serikali ilipambana vikali na matukio haya mapya ya vurugu. Siku zilizofuata Polisi walipelekwa kupekua nyumba hadi nyumba wakiwasaka viongozi wa uhalifu huo. Wakati viongozi wanne wa Dayosisi ya Mlima Meru wakishitakiwa kwa kosa la kuanzisha fujo, katika Kata ya Poli watu 42 walikamatwa, na familia nyingi zilikimbia makazi yao. Msako kama huu ulifanywa katika vijiji vingi hasa kule Ndatu na Akeri. Jumamosi ya tarehe 17 Julai 1993, Polisi wakiwa kwenye magari yao ya doria, walipita kwenye ile barabara ya changarawe ya Kilala. Ili kuwazuia wasiweze kurudia njia hii, baadhi ya watu waliweka magogo njiani, hata hivyo bila mafanikio makubwa. Kule Ndatu Polisi walimkamata kila mtu waliyemkuta: mkubwa kwa mdogo, waume kwa wake, na kuwasweka rumande kwa usiku mmoja na kuwaachilia kesho yake. Kule Akeri askari walilizingira kanisa wakati wa ibada na kuwachukua waumini waliokuwa wakisali wapatao 20, na wakawapeleka rumande kwa usiku wote. Wakati huu wale viongozi wa Dayosisi ya Mlima Meru bado walikuwa gerezani.

Haijulikani kama ni baada ya kipigo kikali au ni kwa kujiuliza wenyewe hatima ya mambo haya ndipo Varwa wengi walianza kuhisi ugumu wa mambo hayo? Walianza kuona wazi kuwa wasingeweza kuendelea tena na matendo yenye kuvunja sheria ambayo hata dhamiri zao zilikataa na pia hawakuwa tena na tumaini la kushinda mapigano ambayo yalikuwa yamewaelemea kwani nguvu ya dola ilikuwa kinyume nao. Zaidi

ya hilo, palikuwa na mabadiliko makubwa ya fikra za watu, mikutano ikafanywa ya kujadili kama waendelee na ugomvi au la. Watu, hasa wanaume, walikutana na kama kawaida walichagua mwenyekiti na katibu wa kikao. Watu walihesabiwa ili waweze kupata koramu inayotosha. Baada ya wajumbe wengi kutoa mawazo yao, kura ilipigwa kwa kunyoosha mikono, na kwa wingi wa kura iliamuliwa kuacha ugomvi. Vijiji vingi katika eneo la Varwa vilikubaliana kwa njia ya kidemokrasia uamuzi wa namna hiyo. Katika Kijiji cha Ndatu, ambapo mimi mwenyewe nilihudhuria, mkutano ulichagua watu wawili ili wakatoe habari za wahalifu kwa Utawala, na pia ujumbe ukapelekwa kwa Mkuu wa Wilaya kuwa raia wa Ndatu tangu sasa wanataka amani na wanakaribisha ziara yake ambayo hapo awali walikuwa wameisusia kwa vile walimuona amekuwa kama adui yao. Baada ya majadiliano, iliamuliwa kuwa katika ujumbe wa namna hii, mshili wa rika ndiye mwakilishi bora zaidi kuliko mshili wa ukoo. Nao mabalozi wote 22 wa nyumba kumi (kati yao mmoja akiwa mwanamke) wakaagizwa kwenda kuhubiri amani kwa familia zile wanazoziwakilisha. Tokea hapo ndipo amani ikawa imerejea tena kwa Varwa angalau katika vitendo vya watu hata kama si katika mioyo yao. Katika hatua kama hii, pongezi lazima zitolewe kwa Varwa kwa hekima yao hiyo. Ingawaje malengo yao yalionyesha bado kutimizwa, hata hivyo katika hali ya kushangaza walifanikiwa kwa njia ya kidemokrasia kusitisha mgogoro wao na kukomesha mapigano miongoni mwao na hivyo kufuata njia ya mafundisho ya Kikristo ambayo wanayaamini sana.

Hata hivyo miezi kumi na nane baadaye ilidhihirika wazi kuwa uhasama uliokuwa umeletwa na mzozo wa Varwa ulikuwa bado haujamalizika kabisa kabisa. Wale waliokuwa wafuasi wa Dayosisi ya Mlima Meru bado waliipinga ile dayosisi rasmi ya

Kilutheri ya Meru. Hivyo, waliunda Kanisa lao wenyewe wakaliita Kanisa la Uinjilisti la Afrika (Africa Mission Evangelism Church, A.M.E.C). Askofu wake, Luka Pallangyo, ambaye mwanzoni alikuwa mchungaji wa Kilutherani wa Jimbo la Meru, alichaguliwa tarehe 27 Novemba 1993. Kama Askofu Pallangyo alivyoeleza, kanisa hili jipya halina tofauti yo yote ya kiimani na Ulutheri, bali tofauti ni kwenye maongozi tu. Kanisa la A.M.E.C, ambalo ni kanisa jipya na lenye jina jipya, linasimama peke yake. Halipo kwenye fungamano la makanisa mengine, na kinyume na kanisa la Kilutheri kanisa hili halipati msaada wowote toka makanisa mengine ya ndani au nje ya Tanzania. Wakati naandika andiko hili, kanisa hili lilikuwa linangojea usajili wa Serikali toka Dar-es Salaam. Wafuasi wa A.M.E.C waliachilia mbali madai yao ya majengo ya makanisa ya Kilutheri, mashamba na mali nyingine zote na kuanza kujenga makanisa yao wenyewe. Kwa mfano, mhisani mmoja wa kanisa hili katika Kijiji cha Ndatu, alitoa sehemu ya shamba lake ambapo walijenga jengo jipya la kanisa la mbao. Sehemu nyingine nyingi kwa Varwa watu walifanya vivyo hivyo.

Kuhusu MESODET, kutokana na vurumahi zilizotokea kwa Varwa, shughuli zake zilisimama kabisa. Mashtaka ya tuhuma za ubadhirifu wa pesa za MESODET yalikuwa yakisubiri hukumu. Mtengano kati ya Kanisa la Kilutheri na MESODET yaelekea ukawa wa kudumu hasa kwa kuwa viongozi wakuu wa MESODET walikuwa wafuasi wa iliyokuwa Dayosisi ya Mlima Meru, na sasa ni wafuasi wa Kanisa la A.M.E.C. Kanisa la Kilutheri liliwafukuza viongozi waliokuwa wa Dayosisi ya zamani ya Mlima Meru kutoka kwenye bodi za Shule inazomiliki. Wakati huo huo, hapo tarehe 6 Januari 1995, MESODET iliitisha mkutano wake mkuu chini ya ule mti maarufu wa *mringaringa* kule Poll ili kurekebisha katiba yake. Kati ya marekebisho yaliyofanywa siku

hiyo ni pamoja na kuiondoa K.K.K.T kama rneneja wa MESODET na pia ulitolewa wito kwa waumini wa madhehbu yote kujiunga na MESODET. Mwishoni wa mkutano huo, ulichaguliwa ujumbe wa watu wanne kwenda kushughulikia kuandikisha katiba mpya ya MESODET kule Dar es Salaam. Ikapendekezwa kukatwe ushuru wa shilingi 100/= toka kila kilo ya kahawa itakayouzwa katika vyama vya msingi vya ushirika, kwa lengo la kupata fedha kiasi cha shilingi milioni 500/= ili zitumike kwa kazi za maendeleo kwa Varwa wote.

Kwa hiyo, MESODET ilijaribu kuhuisha kazi zake kwa upya japo kulikuwepo bado na mashaka kadhaa. Ni wazi kuwa viongozi wakuu wa MESODET walikuwa wafuasi wa ile iliyokuwa Dayosisi ya Mlima Meru. Ingawaje wanadai kuwa wao ni wawakilishi wa Varwa wote, je, ni watu wote watakaowaona hivyo? Na je, wao wataweza kweli kutoa huduma kwa maslahi ya watu wote? Usimamizi wa shilingi za Kitanzania milioni 500/= zinazotarajiwa kukatwa toka kwenye mauzo ya kahawa unaleta maswali magumu hasa kutokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya mchango huo imelengwa kutumika kwa maendeleo ya shule za sekondari ambazo zinasimamiwa na Kanisa la Kilutheri. Je, MESODET ndiyo itakayosimamia matumizi ya bajeti hiyo? Hapa ikumbukwe kwamba baadhi ya viongozi maarufu wa MESODET walifukuzwa na Kanisa la Kilutheri kutoka kwenye bodi za shule hizi. Swali hili bado halijapata ufumbuzi yakinifu.

Kwa upande wa Kanisa la Kilutheri, tangu kumalizika kwa yale mapambano ya wazi, linaonekana kupata utulivu. Wachungaji wao hutembelea familia mbali mbali ili kujaribu kurudisha tena imani na uhusiano mzuri ikiwa ni pamoja na kushawishi watu kurudi tena kwenye kundi lao. Wachungaji wengi wapya wa Varwa walibarikiwa hivi karibuni ili

kuchukua nafasi za uchungaji katika kabila lao, jambo ambalo limefanya uwiano wa wachungaji wazawa katika Dayosisi ya Meru kuwa mkubwa zaidi kulinganisha na Dayosisi nyingine za Kilutheri Tanzania. Mtindo huu waweza kuchochea utulivu wa ndani baada ya muda fulani; na hata kama kwa sasa bado hali inaonekana kuwa ngumu kiasi fulani, bado makanisa ya Kilutheri si tupu hata kidogo.

## HITIMISHO

Ni wazi kuwa kwa sasa ule upekee wa awali wa Kanisa la Kilutheri kwa Varwa umefikia mwisho wake, na hii ni mojawapo ya matokeo makubwa ya mzozo wake wa kidini. Varwa sasa wamejitoa katika ukiritimba wa dhehebu moja na kuingia kwenye hali mpya ya mtandao wa uhuru wa madhehebu mengi, japokuwa kuwepo kwa wachungaji wengi wazawa katika Kanisa la Kilutheri kwaweza kuwafanya baadhi ya waumini kurudi katika Kanisa hili. Kwa ujumla, licha ya utulivu unaoonekana kuwepo kwa sasa, adhari nyingine kubwa na ya muda mrefu iliyojitokeza katika mzozo huu ni kule kuruvugika kwa mahusiano ya kijamii miongoni mwa Varwa. Chuki yaelekea itadumu kwa muda mrefu katika familia moja na hata kati ya majirani kwani kila familia na kila kaya ina wafuasi katika pande zote hizi mbili. Hali iko hivyo hivyo kwa Dayosisi hizi mbili (sasa makanisa) zilizogongana ambapo zote zilikuwa na matajiri, wasomi na hata maskini kwa kiasi kikubwa. Hakuna sababu halisi za kijamii zilizochangia mzozo huu, ziwe ni kutokana na wazazi, marika, ukoo, utajiri au hata kiwango cha elimu. Kila mtu anaonekana alichagua kambi yake kwa kufuata dhamiri ya moyo wake mwenyewe. Mshikamano wa kijamii haukusaidia chochote, na mzozo huu ndio hasa ukaharibu kabisa mshikamano huu na hata kuleta machungu kwa kila mtu.

Zaidi ya hayo yote, tumeona pia jinsi ambavyo matukio hayo yalihusisha taasisi kadhaa. Ni pale tu kura ya mwisho ilipopigwa ya kusimamisha ugomvi, ndipo taasisi hizi ziliporudisha tena utendaji wake wa kawaida, isipokuwa MESODET. Hata hivyo, ni dhahiri kabisa kwamba uchungu uliopo dhidi ya Serikali na wachungaji utakwamisha utendaji

kazi wa taasisi hizi. Kuhusu mamlaka ya Mshili Mkuu, tumeona kuwa mamlaka yake yaliathiriwa sana kwani alikosa uwezo katika kupatanisha pande hizi mbili zilizokuwa zinagombana. Ukitafakari mwendo mzima wa matukio ya mzozo huu utaona kuwa Mshili Mkuu alishughulika kwa kiwango kidogo mno, na hali nzima ilimfanya apoteze zaidi ushawishi wake. Kutokana na afya yake Mshili Mkuu ilibidi ajiuzulu, na mwingine mpya, Bethueli Paulo Kaaya, alichaguliwa hapo mwaka 1995. Kutokana na upya wake, pengine huyu Mshili Mkuu mpya huenda akafanikiwa kutegua kitendawili hiki cha mshikamano wa jamii ya Varwa na kurudisha hali kama pale mwanzoni.

Kwa mtazamo wa kiutawala, mzozo huu umeibua dhana ya mipaka ya kiutawala iliyorithiwa toka ukoloni, kama ile ya utawala wa kijamii (kufuata mipaka ya vijjiji) na katika dini (mgawanyo wa sharika zikifuata kwa kiasi fulani mipaka ya vijiji). Msingi mkubwa wa mipaka ya kijiografia unafuata vijiji. Ni kijiji fulani ndicho kilichoamua kwa njia ya kura juu ya hatua zilizopaswa kuchukuliwa; ilikuwa ni kwenye ngazi ya kijiji ndipo ulinzi wa pamoja ulipoanzishwa; na pia ilikuwa ni kwenye ngazi ya kijiji ndipo maamuzi yalifikiwa kwa njia ya kidemokrasia kuhusu kusitisha ugomvi na kumaliza uadui. Kwa hali hiyo basi, kijiji sio tu ni eneo la kiutawala, bali pia ni shina muhimu la umoja wa kijamii.

Kwa ujumla mambo yaliyotokea katika mzozo huu ni mengi na yenye utata, na hivyo yasiyoweza kutabirika. Uchambuzi wa kina kuhusu mzozo mzima ni mgumu hasa ukizingatia ukweli kuwa kuna hali tofauti kutoka kijiji kimoja hata kingine miongoni mwa Varwa. Kwa mfano, Kanisa hili la AMEC limejiimarisha zaidi huko pande za maghanbi kwa-Varwa. Je, litaweza kufanikiwa kushawishi waumini wote na

kuleta maendeleo ya kiumoja katika eneo lote la Varwa? Rasilimali zake kwa sasa hivi bado ni dhaifu hasa kulinganisha na rasilimali imara na za muda mrefu za kanisa la Kilutheri ambazo zinatokana na utajiri wake pamoja na misaada ya wafadhili wa nje.

Upo wasiwasi mkubwa juu ya hatima ya baadaye ya MESODET. Je, itaweza kweli kusimamia shughuli zote za maendeleo kama inavyokusudiwa? Uhasama wake na Kanisa la Kilutheri bado kabisa kumalizika, na huu waweza kuweka kikwazo kikubwa kwenye maendeleo ya Varwa. Zaidi ya hayo, Varwa, kama wakulima wa kahawa, hutegemea sana mauzo ya zao hili katika kuchangia maendeleo yao. Kwa hiyo, usimamizi wa vyama vya msingi vya ushirika vya kahawa ni jambo muhimu sana. Je, vyama hivi vya ushirika bado vitachangia MESODET kama inavyotarajiwa? Ni dhahiri kuwa utafiti wa kina unahitajika kuhusu mahusiano kupitia vyama hivi vya ushirika. Hili ni jambo jingine la msingi katika kufahamu zaidi juu ya maendeleo ya Varwa kiuchumi na kisiasa, mambo ambayo yana uhusiano mkubwa.

## ORODHA YA VITABU

Catherine Baroin ni mjumbe katika shirika la utafiti wa sayansi ya jamii, CNRS, Ufaransa.


1. John Iliffe, *A Modern History of Tanganyika* (Cambrige University Press, Cambridge, 1979).
2. A.S.Mbise, 'The Evangelist Matayo Leveriya Kaaya', katika John Iliffe (ed), *Modern Tanzanians - a volume of biographies* (East African Publishing House, Nairobi, 1973), uk. 27-42.
3. C.K Omari, 'Episcopacy, a Sociological Trend in the Lutheran Church in Tanzania', katika *Africa Theological Journal,* Makumira (Tanzania), 16 (1987), uk.. 4-12.
4. S. F. Moore and P. Puritt, *The Chagga and Meru of Tanzania,* (International African Institute, Ethnographic Survey of Africa, 18, London, 1977).
5. S.E Nnko, 'The Interdenominational Conflict Within the Meru District of the ELCT - Northern Diocese' (Makerere University, unpublished Diploma of theology, Archives of the Makumira Lutheran Theological College in Tanzania, 1980).
6. Gerard Philippson,' 'Les populations', katika Batibo and Martin, *Tanzanie -L'ujamaa face aux realites,* p.43.
7. P.H. Gulliver, *Social Control in an African Society. A study of the Arusha: agricultural Maasai of Northern Tanganyika* (Routledge and Kegan Paul, London, 1963).
8. J.Bayart and A.Mbembe, 'La bataille de I'archidiocese de Douala', *Politique Africaine* 35, *L'argent de Dieu* (1989), uk.79.
9. *Business Times,* 25 December 1992.

10. Kirilo Japhet and Earl Seaton, *The Meru Land Case* (East African Publishing House, Nairobi, 1967).
11. *The Express,* 23-29 April 1992.
12. *Daily News,* 3 June 1992
13. Barua ya Askofu Kolowa iliyochapishwa kwenye gazeti la KKKT la U*moja,* 1 & 2, (1992) uk. 32.
14. Thomas Spear (ed.) *Evangelisch-Lutherisches Missionsblatt. Extracts on Arusha and Meru, 1897 - 1914,* kilichotafsiriwa na C. M. Murphy (African Studies Program, University of Wisconsin-Madison, 1995), uk. 40.
15. Gazeti la *Uhuru* (la CCM), 9 April 1993.
16. Gazeti la U*huru,* 15 April 1993.